**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**2020 - 2025**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Zubeir Ali Maulid | - | SPIKA |
| 2. | Mhe. Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/Nafasi za Wanawake |
| 3. | Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | - | Jimbo la Dimani |
| 4. | Mhe. Shaaban Ali Othman | - | Jimbo la Mpendae |
| 5. | Mhe. Hemed Suleiman Abdulla | - | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Uteuzi wa Rais |
| 6. | Mhe. Mudrik Ramadhan Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji/ Jimbo la Bububu. |
| 7. | Mhe. Masoud Ali Mohammed | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Ole. |
| 8. | Mhe. Haroun Ali Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora/Jimbo la Makunduchi. |
| 9. | Mhe. Jamal Kassim Ali | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Fedha na Mipango/Jimbo la Magomeni. |
| 10. | Mhe. Dkt Khalid Salum Mohamed | - | MBM/Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi/Jimbo la Donge. |
| 11. | Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan | - | MBM/Waziri wa Kilimo, |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo/Jimbo la Paje |
| 12. Mhe. | Simai Mohammed Said | - | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Tunguu |
| 13. Mhe. | Tabia Maulid Mwita | - | MBM/Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo/ Uteuzi wa Rais |
| 14. Mhe. | Riziki Pembe Juma | - | MBM/Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi/ Nafasi za Wanawake |
| 15. Mhe. | Rahma Kassim Ali | - | MBM/Waziri Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi/Nafasi za Wanawake |
| 16. Mhe. | Suleiman Masoud Makame | - | MBM/Waziri wa Maji, Nishati na Madini/Jimbo la Chonga |
| 17. Mhe. | Abdulla Hussein Kombo | - | MBM/Waziri wa Uchumi wa Bluuu na Uvuvi /Jimbo la Mkoani |
| 18. Mhe. | Lela Muhamed Mussa | - | MBM/Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale/Nafasi za Wanawake |
| 19. Mhe. | Abdalla Abasi Wadi | - | Jimbo la Nungwi |
| 20. Mhe. | Ali Abdulgulam Hussein | - | Jimbo la Jang'ombe |
| 21. Mhe. | Ali Suleiman Ameir | - | Jimbo la Pangawe |
| 22. Mhe. | Ameir Abdalla Ameir | - | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 23. Mhe. | Anna Athanas Paul | - | Uteuzi wa Rais |
| 24. Mhe. | Asha Abdalla Mussa | - | Jimbo la Mahonda |
| 25. Mhe. | Azza Januar Joseph | - | Nafasi za Wanawake |
| 26. Mhe. | Bahati Khamis Kombo | - | Jimbo la Chambani |
| 27. Mhe. | Bakar Hamad Bakar | - | Jimbo la Wawi |
| 28. Mhe. | Bihindi Hamad Khamis | - | Nafas iza Wanawake |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 29. Mhe. | Fatma Ramadhan Mohamed (Mandoba) | | Nafasi za Wanawake |
| 30. Mhe. | Habibu Ali Muhamed | - | Jimbo la Mtambwe |
| 31. Mhe. | Haji Omar Kheri | - | Jimbo la Tumbatu |
| 32. Mhe. | Haji Shaaban Waziri | - | Jimbo la Uzini |
| 33. Mhe. | Hamza Hassan Juma | - | Jimbo la Kwamtipura |
| 34. Mhe. | Harusi Said Suleiman | - | Jimbo la Wete |
| 35. Mhe. | Hassan Hamad Omar | - | Jimbo la Kojani |
| 36. Mhe. | Hassan Khamis Hafidh | - | Jimbo la Welezo |
| 37. Mhe. | Hudhaima Mbarak Tahir | - | Nafasi za Wanawake |
| 38. Mhe. | Hussein Ibrahim Makungu | - | Jimbo la Mtoni |
| 39. Mhe. | Juma Makungu Juma | - | Jimbo la Kijini |
| 40. Mhe. | Juma Ali Khatib | - | Uteuzi wa Rais |
| 41. Mhe. | Issa Haji Ussi Gavu | - | Jimbo la Chwaka |
| 42. Mhe. | Kombo Mwinyi Shehe | - | Jimbo la Wingwi |
| 43. Mhe. | Machano Othman Said | - | Jimbo la Mfenesini |
| 44. Mhe. | Maryam Thani Juma | - | Jimbo la Gando |
| 45. Mhe. | Mihayo Juma Suleiman | - | Jimbo la Mwera |
| 46. Mhe. | Miraji Khamis Mussa | - | Jimbo la Chumbuni |
| 47. Mhe. | Mohamed Mgaza Jecha | - | Jimbo la Mtambile |
| 48. Mhe. | Mohamed Ahmada Salum | - | Jimbo la Malindi |
| 49. Mhe. | Mtumwa Peya Yussuf | - | Jimbo la Bumbwini |
| 50. Mhe. | Mussa Foum Mussa | - | Jimbo la Kiwani |
| 51. Mhe. | Mwanaidi Kassim Mussa | - | Nafasi za Wanawake |
| 52. Mhe. | Mwantatu Mbarak Khamis | - | Nafasi za Wanawake |
| 53. Mhe. | Mwanajuma Kassim Makame | - | Nafasi za Wanawake |
| 54. Mhe. | Dkt. Mwinyi Talib Haji | - | Mwanasheria Mkuu |
| 55. Mhe. | Nadir Abdullatif Yussuf | - | Jimbo la Chaani |
| 56. Mhe. | Nassor Salim Ali | - | Jimbo la Kikwajuni |
| 57. Mhe. | Nassor Ahmed Mazrui | - | Uteuzi wa Rais |
| 58. Mhe. | Omar Said Shaaban | - | Uteuzi wa Rais |
| 59. Mhe. | Panya Ali Abdalla | - | Nafasi za Wanawake |
| 60. Mhe. | Rukia Omar Ramadhan | - | Jimbo la Amani |
| 61. Mhe. | Saada Ramadhan Mwendwa | - | Nafasi za Wanawake |
| 62. Mhe. | Dkt. Saada Mkuya Salum | - | Uteuzi wa Rais |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **63.** | **Mhe.** | **Saidi Saleh Salim** | **-** | **Jimbo la Tumbe** |
| **64.** | **5Mhe.** | **Sabiha Filfil Thani** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **65.** | **Mhe.** | **Salha Mohamed Mwinjuma** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **66.** | **Mhe.** | **Salma Mussa Bilal** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **67.** | **Mhe.** | **Suleiman Makame Ali** | **-** | **Jimbo la Ziwani** |
| **68.** | **Mhe.** | **Suleiman Haroub Suleiman** | **-** | **Jimbo la Kiembe Samaki** |
| **69.** | **Mhe.** | **Sulubu Kidongo Amour** | **-** | **Jimbo la Mkwajuni** |
| **70.** | **Mhe.** | **Shadya Mohamed Suleiman** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **71.** | **Mhe.** | **Shamata Shaame Khamis** | **-** | **Jimbo la Micheweni** |
| **72.** | **Mhe.** | **Shaib Hassan Kaduara** | **-** | **Jimbo la Chake Chake** |
| **73.** | **Mhe.** | **Yahya Rashid Abdulla** | **-** | **Jimbo la Kwahani** |
| **74.** | **Mhe.** | **Yussuf Hassan Iddi** | **-** | **Jimbo la Fuoni** |
| **75.** | **Mhe.** | **Zaina Abdalla Salum** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **76.** | **Mhe.** | **Zawadi Amour Nassor** | **-** | **Jimbo la Konde** |

| | | |
|---|---|---|
| **Ndg. Raya Issa Msellem** | **-** | **Katibu** |

**Kikao cha Nne – Tarehe 15 Februari, 2021**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua*

**TANGAZO**

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa, kabla ya kuanza naomba nitoe tangazo linalotokana na chumba chetu cha masuala ya vipaza sauti, wameomba sana Waheshimiwa Wajumbe wanapotumia vipaza sauti hivi waviweke kidogo upande wasiweke *direct*. Kwa sababu pindipo unapoweka *direct* sauti kule inatoka vyengine inakuwa haisikiki vizuri. Kwa wanatuomba kwamba hata ukiweka upande hivi utakuwa unasikilikana kwa ufasaha sana. Hilo ni moja.

Lakini vile vile la pili wamekumbusha wakati tunapozigonga meza wakati tumefurahi au tuna jambo lolote ambalo tunaliunga mkono wanaomba sana meza hizi zisipigwe kwa nguvu, kwa sababu *wirering* yenyewe iko *very sensitive*. Kwa maana ya kwamba iwapo itatikisika kidogo maana yake tutakosa kufanya shughuli zetu. Kwa hivyo nawaomba sana hayo tuwe na tahadhari nayo.

**TAARIFA YA SPIKA**

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe katika kikao cha Baraza cha tarehe 11 Februari, 2021 Mhe. Asha Abdalla Mussa aliuliza swali la nyongeza lililotokana na suala la msingi namba 20. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ aliahidi kutoa jibu la suala hilo kwa maandishi.

Sasa namuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ asome jibu la suala hilo lililoulizwa na Mjumbe huyo. Mhe. Waziri karibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza lililoulizwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa Mwakilishi wa Jimbo la Mahonda na kuahidi kuleta kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha orodha za barabara za ndani zilizofanyiwa upembuzi yakinifu zenye jumla ya kilimota 242 Unguja na Pemba kama nilivyowasilisha katika maandishi na nitawasilisha kwako orodha hii.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mheshimiwa.

Waheshimiwa orodha iko hapa na ni orodha ndefu kwa hiyo itakuwa sio rahisi kuisoma yote. Kwa hiyo, yule ambaye atataka orodha hii basi ataweza kupatiwa na meza ya katibu lakini na

Mhe. Asha Abdalla Mussa tayari ameshapatiwa orodha hiyo. Tunashukuru sana Mhe. Waziri. Tuendelee.

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango):** Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Hati mezani Hotuba ya Muelekeo wa Mpango wa Taifa kwa mwaka 2021/2020 na waraka wa Mpango wa Bajeti. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Anna Athanas Paul (Kny. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti):** Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Muelekeo wa Mpango wa Taifa kwa mwaka 2021/2022 na Waraka wa Mpango wa Bajeti. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

## MASWALI NA MAJIBU

### Nam. 8

### Kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo wa Watu wenye Mahitaji Maalum

**Mhe. Zaina Abdalla Salum (Kny. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis): –** Aliuliza**:**

Serikali katika kuhakikisha watu wenye mahitaji maalum wanafaidika na huduma muhimu kwa lengo la kupata maendeleo, imeanzisha mfuko wa maendeleo kwa watu wenye mahitaji maalum.

(a) Ni maeneo gani hadi sasa yameweza kufaidika na mfuko huo.

(b) Je, mfuko huo umewafikia watu wenye mahitaji maalum wangapi Unguja na Pemba.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais) –** Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 8 lenye kifungu (a) na (b) naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, lengo la mfuko huu ni kuwawezesha Watu wenye Ulemavu kupata Haki na Fursa pamoja na kuondolea vikwazo vinavyosababisha wenzetu wenye ulemavu kushindwa kupata mikopo na rukuzu lakini pia kupata huduma katika elimu na matibabu.

Mhe. Naibu Spika, Watu wenye Ulemavu wanatambuliwa na Sera ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2018, Sheria ya Watu wenye Ulemavu Haki na Fursa Nam. 9 ya mwaka 2006 na Mkataba wa Kimataifa wa haki na Fursa za Watu wenye Ulemavu.

Ibara ya 27 ya Mkataba wa Kimataifa wa haki za Watu wenye Ulemavu unahitaji kuimarisha na kukuza fursa za watu wenye Ulemavu kujiajiri wenyewe na kuajiriwa lakini pia kuanzisha na

kuendesha shughuli za ujasiriamali, kuanzisha vyama vya ushirika na mtu binafsi kujianzishia biashara yake mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, katika kulitambua hili, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Idara ya Watu wenye Ulemavu, katika kifungu 38 cha Sheria ya Watu wenye Ulemavu Haki na Fursa Nam. 9 ya mwaka 2006 ilianzisha Mfuko wa Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu, kwa lengo la kukidhi vigezo vya kikanda na kimataifa ili kumiarisha haki za watu wenye ulemavu nchini kwetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar unasimamiwa na Sheria, Kanuni na Muongozo wa matumizi ya Mfuko. Kwa sasa Mfuko huu umeshatoa ruzuku ya elimu na ruzuku kwa ajili ya matibabu. Aidha, Mfuko huu tayari umezifikia Wilaya zote 10 za Unguja na Pemba kwa kutoa mikopo kwa wajasiriamali mbali mbali na umefikiwa katika Sheria 63 za Unguja na Pemba. Mhe. Naibu Spika, Vikundi vilivyonufaika ni vikundi vya uzalishaji wa mboga mboga, uvuvi kwa maana ya boti ya kuvulia, usukaji wa mikoba, makawa, uzalishaji wa mafuta ya kujipaka, sabuni, uanikaji wa dagaa, ufugaji wa kuku wa mayai, ufugaji wa kuku wa nyama na ununuzi wa gari ya kubebea mizigo.

(b) Mhe. Spika, hadi sasa Mfuko umewafikia jumla ya watu 94, wenye Ulemavu kwa Unguja na Pemba. Kati ya hao Unguja ni 57 na Pemba ni 37.

Miongoni mwao, watu wenye ulemavu 82 wamepatiwa mikopo ambapo kutoka Unguja ni 47 (30 wanaume na 17 wanawake) na Pemba ni 32 (wanaume 22 na wanawake 10). Aidha vikundi vitatu kutoka Unguja navyo vilipatiwa mikopo hii.

Mhe. Naibu Spika, aidha, jumla ya watu 6 wenye ulemavu wamepatiwa ruzuku za elimu wanawake 3 kutoka Unguja na wanaume 3 kutoka Pemba. Kwa upande wa ruzuku za matibabu watu wenye ulemavu 6 wamenufaika na ruzuku hiyo, kati yao watu 4 kutoka Unguja (wanawake 2 na 3 wanaume) na Pemba 2 (mwanamme 1 na mwanamke 1).

**Mhe. Zaina Abdalla Salum:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa tena nafasi ya kuuliza swali la nyongeza:-

Mhe. Naibu Spika, kutokana na maelezo ya Mhe. Waziri na majibu yake mazuri nimeona kwamba kwa kanuni na Sheria ya watu wenye mahitaji maalum au watu wenye ulemavu kuwa ameifahamu vizuri.

Lakini kutokana na majibu yake ya msingi ambayo aliyoelezea na mimi sasa nataka nimuulize swali la moja la nyongeza:-

Mhe. Naibu Spika, kwa kupitia majibu yake la swali la msingi ambalo alilojibu kwamba anawapatia mikopo watu wenye ulemavu au wenye mahitaji maalum ili kujikwamua na ukakasi wa kimaisha.

(a) Nataka kujua tu kwamba ni kiasi gani cha fedha ambacho kinachotolewa katika mikopo ile.

(b) Lakini pia hao aliowasaidia katika masuala ya elimu pamoja na afya, ni kiasi gani cha fedha ambacho huwa kinatolewa kuwasaidia watu hao kwa elimu? Ahsante Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais):**

(a) Mhe. Naibu Spika, hadi sasa mikopo iliyotolewa ni ya wastani milioni mia moja na arubaini na moja laki mbili tisini na sita elfu na hiyo inatolewa kufuatana na mahitaji ya muombaji. Lakini ikiwa muombaji ni mtu binafsi anaweza kuomba kima chochote hadi kima cha shilingi laki saba, lakini ikiwa ni kikundi anaweza kukopa kima chochote hadi shilingi milioni kumi na kwa wastani karibu tuna *average* ya mkopo wa shilingi milioni moja laki saba kwa wakopaji wote waliowahi kukopa katika mkopo huu.

(b) Pili aliuliza wastani wa mikopo inayotolewa kwa ruzuku ya elimu nayo inategemea mahitaji. Lakini kwa wastani waliopewa ni milioni moja laki mbili na hamsini elfu.

**Mhe. Anna Athanas Paul:** Mhe. Naibu Spika, naomba kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa majibu yake mazuri, lakini nilikuwa nina ombi langu la ziada hizi *data* alizozitoa vikundi kwa watu binafsi mbali mbali ningeomba hivi vikundi tukatajiwa viko wapi ili tuweze labda kama tunahitaji kuviona tuweze kuviona kwa urahisi kikundi gani jina lake na kiko sehemu gani. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais):** Mhe. Naibu Spika, kwa vile sina takwimu hapa naomba uniruhusu takwimu hizo nizilete kwa maandishi.

**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake ya ufasaha. Lakini pia Mhe. Waziri katika majibu yako umesema watu 94 wenye mahitaji maalum ndio waliopata mkopo.

(a) Mhe. Naibu Spika, idadi hii ni ndogo sana ukilinganisha na watu wenye ulemavu.

(b) Je, kwa mwaka huu wa fedha wizara yako hii imejipangaje katika kuwapa mikopo watu hawa wenye mahitaji maalum. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais):**

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Shadya swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, kwanza nakiri kima kilichotoka ni kidogo na idadi ya waliofaidika ni kidogo. Lakini haitolewi kwa watu wenye ulemavu mikopo hii, kwa sababu watu wenye ulemavu kwa mujibu wa *data base* wako karibu elfu nane mia tatu na thalathini na tatu.

(b) Mikopo hii inatolewa kwa masharti na lazima kwanza anapata mikopo hii awe tayari kupokea mikopo hii kwa ajili ya kujiendeleza kiuchumi awe mtu mwenye ulemavu awe Mzanzibari lakini awe tayari kujiendeleza na tayari anajishughulisha na shughuli za uchumi.

Kwa hivyo, suala la mwazo wizara hii itakalofanya ni kushajihisha watu wenye ulamavu kujiingiza katika masuala ya kujiendeleza kiuchumi ili waweze ku-*qualify* kupata mikopo hii. Lakini pia urudishaji wa mkopo huu umeonekana kwamba uko katika kiwango cha chini sana zimetoka karibu milioni mia moja na arubaini na moja lakini madurisho ni milioni kumi na nne sawa na asilimia 10.2.

Sasa ni muhimu sana kuhakikisha hawa wanaonufaika na wizara italifanyia kazi hilo waweze kujiendeleza na kupata faida ili waweze kurudisha mikopo hii wanufaike watu wengine. Lakini serikali haitasita kuongeza kima cha fedha pale mkopo huu ukiwa unaendelea vizuri.

**Nam. 1**

**Gofu la Mkamandume liliopo katika Shehia ya Dodo**

**Mhe. Mohamed Mgaza Jecha (Kny. Mhe. Bahati Khamis Kombo) –** Aliuliza**:**

Gofu la Mkamandume lipo katika Shehia ya Dodo na ukitaka kulitambua kwa namna nzuri basi lazima utembelee katika msikiti mkongwe uliopo Mitamani shehia ya Dodo lakini hivi sasa linaonesha lipo katika shehia ya Pujini.

(a) Je, ni vigezo gani vilivyotumika kutolewa Gofu hilo shehia ya Dodo na kupelekwa shehia ya Pujini.

(b) Kwa kuwa limepelekwa Pujini na wananchi wa Dodo ndio asili yao, si tunawakosesha haki zao za maendeleo yanayotokana na gofu hili.

(c) Je, wakati wa maamuzi hayo wananchi wa Dodo na kamati yao ilipewa taarifa.

**Mhe. Waziri Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ -** Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 1 lenye klifungu (a), (b) na (c) na kabla kumjibu naomba maelezo mafupi kuhusiana na Shehia pamoja na mipaka yake kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 mwenye mamlaka ya kugawa Mikoa, Wilaya na Shehia ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mnamo tarehe 08 Mei 2015, Serikali ilitangaza kwenye Gazeti Rasmi la Serikali Shehia 388 kwa mujibu wa Mamlaka iliyowekwa kwenye kifungu cha 2(a) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 toleo la mwaka 2010 na kifungu cha 4 cha Sheria nambari 8 ya mwaka 2014 cha Sheria ya Tawala za Mikoa.

Baada ya kutangazwa kwa Shehia hizo 388, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ilitakiwa kwenda kuweka alama za mipaka hiyo, kwa mujibu wa ramani ya Zanzibar iliyopo. Hivyo, agizo hilo lilitekelezwa kuanzia mwaka 2018 na kumalizika mwanzo ni mwa mwaka 2020.

Mhe. Naibu Spika, Serikali ililazimika kuweka alama za mipaka ya Shehia kwa sababu kwa muda mrefu mipaka ya Shehia haikuwa ikifahamika kwani wananchi na viongozi walikuwa wakitafsiri mipaka ya Shehia hizo kwa mazoea badala ya uhalisia uliowekwa kwa mujibu wa Sheria. Hivyo, ifahamike kwamba zoezi lililofanyika halikuwa ni la kuweka mipaka mipya ya Shehia, halikuwa ni la kuleta ugomvi wa watu, wala halikuwa kwa sababu yoyote ile isipokuwa ni kuweka alama ili kila mmoja aifahamu mipaka ya Shehia yake. Aidha, lengo la kuweka alama hizo katika ngazi ya Shehia ni kuimarisha mfumo wa utendaji kazi na utoaji wahuduma za umma kwa usahihi na uwazi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa kwa ruhusa yako naomba kujibu swali nambari 1lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, vigezo vilivyotumika la Gofu la Mkamandume kutolewa kwenye Shehia ya Dodo na kupelekwa Shehia ya Pujini ni ramani ya Zanzibar tokea asili pamoja na uwezo aliopewa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kikatiba na kisheria kuigawa Zanzibar kimipaka ya Mkoa, Wilaya na Shehia kama atavyoona inafaa.

(b) Mhe. Naibu Spika, mipaka ya Shehia haihusishwi na kuhamisha umiliki wa rasilimali ya mtu, taasisi au Shehia kwa maana mtu, taasisi au Shehia wanaruhusika kumiliki rasilimali iliyopo katika Shehia yoyote la msingi utaratibu wa Sheria ufuatwe katika umiliki ambao kwa sasa Gofu la Mkamandume linamilikiwa na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale. Hivyo, wananchi wa Dodo hawawezi kukosa haki zao za maendeleo yanayotumika na Gofu la Mkamandume ambalo lipo kwa faida ya wananchi wote wa Zanzibar.

(c) Mhe. Naibu Spika, wakati wa maamuzi hayo wananchi wa Dodo na Kamati yao walipewa taarifa na kuhusishwa katika hatua ya kuweka alama na kutambua mipaka hiyo ambapo pia Shehia ya Dodo ilihamishwa kutoka Wilaya ya Chake Chake na kuwa kwenye Wilaya ya Mkoani.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Mhe. Naibu Spika, naitwa Mhe. Suleiman Makame Ali, Mhe. Naibu Spika nadhani hakuna swali la Mhe. Mwantatu katika order paper angalia vizuri.

**Mhe. Naibu Spika:** Samahani nimefungua ukurasa ule ule wa mwanzo, tunakwenda Wizara ya kilimo Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Mhe. Habib Ali Mohammed.

**Nam. 66**

**Utoaji wa Hati Miliki Katika Mashamba ya Serikali**

**Mhe. Habib Ali Mohamed -** Aliuliza:

Kwa kuwa maisha ya mtu hutegemea rasilimali aliyonayo ambapo watu wengiwa Zanzibar,hasa kisiwa cha Pemba hutumia mashamba yao kujipatia riski . Suala hili limetoa majonzi na masikitiko makubwa kwa wananchi ambapo Serikali ilichukua mashamba ya mikarafu unakuyakodisha mashamba bila yakuwazingatia wahusika.

Je, Serikali italitatuajesuala la umiliki wamashamba na kuhakikisha kwamba mwenye haki ndiye anayepewa hakiyake.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo** - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 66, kwanza naomba kutoa maelezo machache kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli maisha ya mtu hutegemea rasilimali aliyonayo ambapo watu wengi wa Zanzibar hasa kisiwa cha Pemba hutumia mashamba hujipatia riziki zao. Ni kweli suala hili limetoa majonzi na masikitiko makubwa kwa baadhi ya wananchi.

Wizara tayari imechukua hatua za kuyatambua jumla ya mashamba 6315 kati ya mashamba 8215 ya eka yaliyokuweko Pemba yaliyokabidhiwa katika Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo. Kati ya mashamba yaliyotambuliwa 1,525 ni yenye mikarafuu ambayo hayana umiliki wa kisheria kwa mujibu wa utaratibu wa eka tatu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

Mhe.Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzbar imetoa idhini ya kuyapima mashamba ya eka ya mikarafuu 732 yaliopo Kisiwani Pemba kwa ajili ya kupatiwa wananchi walioyaomba mashamba hayo. Kati ya mashamba hayo, mashamba 70 yapo katika Wilaya ya Micheweni, mashamba 218 Wilaya ya Wete, mashamba 140 Wilaya ya Chake Chake na mashamba 304 Wilaya ya Mkoani. Aidha, kazi ya upimaji wa mashamba hayo umekamilika kwa Wilaya ya Micheweni na inaendelea na Wilaya yaWete, jumla ya mashamba 169 (Wete mashamba 114 na Micheweni 55) tayari yameshapimwa kwa kushirikiana na Wizara ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, imo katika hatua za mwisho za matayarisho ya kutaka kuyakabidhi mashamba 55 kwa wananchi kwa Micheweni ambayo tayari yameshapimwa. Ahsante.

**Mhe. Habib Ali Mohammed:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza, kwa mujibu ya serikali ya awamu ya nane inayoongozwa Mhe. Dokt Hussein Ali Mwenyi na Makamu wake Wawili Maalim Seif Sharif Hamad na Mhe. Hemed Suleiman Abdulla inatilia mkazo uendelezaji maeneo ambayo yako wazi ya wawekezaji ardhi na

mashamba. Wako baadhi ya wananchi ambao wamepewa ekari tatu na wameshindwa kuyaendeleza mashamba hayo hawayatunzi vizuri wameyatekeleza je, serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba mashamba yale wanapewa watu ambao wapo tayari kuyaendeleza kwa maslahi ya Taifa.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:** Mhe. Naibu Spika, naomba ruhusa ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kwamba kuna mashamba ambayo wamepewa watu lakini hawayahudumii, mashamba hayo kupitia kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya tutayatathmini na kuona kweli hayatumiki ili kwa wale ambao wanahitaji mashamba hayo waweze kupewa kutokana na maombi kupitia kwa Mkuu wa Wilaya na Mkoa hadi kufikia katika Wizara yetu ahsante Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Issa Haji Ussi:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, nikushkuru kwa kunipa nafasi na naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri yenye kutoa ufafanuzi wa kutosha, pamoja na pongezi hizo naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ametueleza kwamba mashamba ameyatambua na wameanza zoezi la kuyapima, lakini mashamba yote kwa ujumla yalikuwa 732 ambayo yamepimwa na kutambuliwa ni mashamba 169 kuna jumla ya mashamba 563 hayajatambuliwa wala hajapimwa.

a) Je, kuna ugumu gani ama kuna tatizo gani lililopelekea zoezi hili ambalo limeanza kitambo kwamba hadi leo hii liwe halijakamilika kuchelewa kuyatambua mashamba haya na kuyapima kunapelekea athari kubwa kama swali la msingi ambalo limeulizwa kwa watu ambao wangeweza kupewa mashamba haya na kuyatumia kwa ajili ya uzalishaji.
b) Zoezi kama hili la kuyatambua mashamba kama haya kwa hapa Unguja litaanza lini na kukamilika lini.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:** Mhe. Naibu Spika, naomba ruhusa ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

a) Kwamba anasema kazi hii ilitolewa zamani lakini mpaka sasa kuna mashamba bado hayajahakikiwa. Mhe. Naibu Spika, kutokana na kazi hii ngumu sio kazi ndogo kwa hivyo uhaba wa wapimaji wa mashamba haya ndio uliosababisha kutotambuliwa lakini bado wizara yangu inaendelea na hatua za haraka kuhakikisha kwamba yanapimwa haraka na yaweze kutambuliwa kwamba ni mashamba ambayo hajaweza kutambuliwa na wizara yangu.

b) Nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba je, Zanzibar swali hili liko namna gani Mhe. Naibu Spika, kwa Zanzibar suala hili bado hatujaendelea nalo kwa sababu hatujapata matatizo au maombi ya kuweza kupatiwa maeneo ya mashamba ya mikarafuu lakini hatua za haraka zitachukuliwa ili kuona kwamba tunayafatilia na kama kuna matatizo basi tuweze kuyatatua lakini mpaka sasa wizara yangu bado haijapata matatizo hayo.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kumuliza Swali la nyongeza Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo. Mhe. Naibu Spika kwanza nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kuweza kujibu maswali yake vizuri na kwa uhakika swali langu liko hapa katika swali lake alipokuwa akijibu amesema

kwamba kwa upande wa Zanzibar alijkusudia Unguja kwamba hiyo kazi haijafanyikia na kwa sababu bado hawajapelekewa hizo changamoto, nilikuwa nataka nimulize Mhe. Waziri anajua kwamba kwa suala la mashamba kwa upande wa Pemba linasimamiwa na Wizara ya Kilimo, Umwsagiliaji, Maliasili na Mifugo, lakini kwa upande wa Unguja linasimamiwa na Wizara ya Ardhi.

a) Je, ategemee hilo suala litakuja kushughulikiwa na Mhe. Waziri wa Ardhi au atakuja kulishughulikia yeye.

b) Kisera na kisheria na hapa labda Mhe. Mwanasheria Mkuu pengine labda anaweza akatusaidia kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni moja Unguja na Pemba kwa nini kwa upande wa Pemba mashamba yanashughulikiwa na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa upande wa Unguja yanasimwamiwa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi wakati tuna nchi moja na serikali moja.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:** Mhe. Naibu Spika, naomba ruhusa ya kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba mashamba haya kwa kweli ni mashirikiano yanafanya mashirikiano kati ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji na Maliasili na Mifugo ikishirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi tunafanya kazi kwa pamoja.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Kajibu (a), (b) niliuliza suala la kisheria na kisera je, wakati tuna serikali moja Zanzibar Unguja na Pemba kuna haja gani au ni haki kwamba Wizara ya Kilimo Pemba ndio inayoshughulikia maswali ya Mashamba wizara ya Ardhi Unguja ndio inayoshughulikia mashamba kwa upande wa Unguja je hili kisheria na kisera ni sahihi.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Nikushukuru sana Mhe. Naibu Spika, nadhani kutokana na swali ambalo limeulizwa na Mhe. Hamza Hassan ni kweli kwamba tukiri kwamba pana mapungufu tokea mwaka 2013, kwa mashamba upande wa Pemba yamepelekwa kwenye Wizara ya Kilimo lakini kwa Zanzibar yako chini ya Wizara ya Ardhi kwa hivyo ni jambo la kisera tutaliangalia ili kuhakikisha kwamba madhali tuna serikali moja tunaenda kama ambayo vile imepangwa kulingana na mashamba.

**Nam. 53**

**Kujenga Skuli ya Kumuenzi Marehemu Sheikh Abeid Amani Amani Karume**

**Mhe. Haji Shaaban Waziri – Aliuliza:**

Serikali katika kuwaenzi Muasisi na Viongozi mbalimbali wa Taifa letu la Zanzibar imekuwa ikijenga vitu mbalimbali kama vile barabara na skuli na kuvipa majina kwa ajili ya kuwaenzi viongozi hao.

(a) Je, hatuoni ipo haja ya kujenga skuli ya ghorofa itakayopewa jina la Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume katika pahali alipoanzia masomo yake Muasisi huyo.

(b) Je, kuna utaratibu gani unaotumika katika kuweka mazingira mazuri ya historia katika skuli zetu.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny.Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali) - Alijibu:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 53 lenye kifungu (a) na (b)kama hivi ifuatavyo:-

(a) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kuwaenzi na kuwakumbuka waasisi wa Taifa letu imezipa majina ya viongozi wa kuuwa Serikali kuanzia awamu ya kwanza mpaka ya saba skuli mbalimbali zilizojengwa Unguja na Pemba. Wizara tayari imeipa jina la Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume skuli mpya ya Ghorofa iliyojengwa katika eneo la Kinuni. Pia,Wizara imetumia jina la marehemu huyo kwa Taasisi ya Karume Sayansi na Teknolojia ambayo awali ilikuwa ikiitwa Chuo cha Ufundi Karume ambacho kiliasisiwa mwaka 1965.

(b) Katika kudumisha historia ya nchi yetu pamoja na viongozi wake, Wizara inaendeleza utamaduni wa kuimba nyimbo za Taifa zenye maudhui ya kihistoria ilikuweka mazingira mazuri ya kihistoria katika skuli zetu. Aidha, Wizara imeweka somo la Historia katika Mtaala wa elimu wa Zanzibar kutoka ngazi ya elimu ya Msingi hadi Sekondari ilikuwawezesha wanafunzi na jamii kujenga uelewa wa nchi na viongozi wao.

**Mhe. Haji Shaaban Waziri:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, namshkuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina swali la nyongeza (a) na (b).

a) Je, Mhe. Waziri mara ngapi amefika katika skuli Mwera ambayo amesoma Rais wetu wa awali.
b) Kwa kuwa Skuli hiyo ni ya muda mrefu na sasa imechakaa mno na ina historia ya muasisi wetu wa nchi hii lini itakwenda kutengenezwa.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny.Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nya nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, ni mara ngapi kutembelea skuli namwambia mara nyingi tu sikumbuki idadi yake ni mara ngapi kwa sababu ni utaratibu wetu katika kuzitembelea skuli zetu. Kwa hivyo tunapokuwa tunakwenda hatuweki kama leo tumekwenda hapa na hapa nikajua ni mara ngapi lakini ni kwamba tayari skuli tumeshaitembelea.
b) Skuli kweli imechakaa kama ambavyo zilivyo skuli nyengine kwa sababu zimejengwa katika miaka ya zamani na kama ambavyo ilivyo taratibu suala la kujenga skuli mpya ya kuifanyia matengenezo skuli ni kwamba inategemea na bajeti yetu, bajeti yetu itakaporuhusu basi na skuli hiyo tutaizingatia katika vipaumbele vyetu. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

**Nam. 67**

## Kukithiri Kwa Vitendo Vya Udhalilishaji Katika Skuli Zetu

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum -** Aliuliza:-

Zanzibar imekuwa ikikabiliwa na wimbi la udhalilishaji wa kijinsia ikiwemo jamii ya watoto na wanafunzi. Aidha, taarifa mbali mbali zinaonesha kuwa, vitendo hivi vya udhalilishaji vimekuwa vikitokea pia baina ya walimu na wanafunzi au wanafunzi kwa wanafunzi wenyewe.

Je, wizara imefanya utafiti wa kina katika skuli zetu kuangalia chanzo cha udhailishaji kwa ujumla.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi: (Kny. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali)** - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 67 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imefanya utafiti wa kina katika skuli zetu kuangalia chanzo cha udhalilishaji katika mwaka 2016. Kabla ya kufanya utafiti huu, kumekuwa na ufuatiliaji na majadiliano ya kina kuhusu udhalilishaji wa watoto hasa baada ya kutungwa sheria ya Kuwalinda Wari na Mtoto wa Mzazi Mmoja, Sheria Namba 4 ya mwaka 2005. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa chanzo cha udhalilishaji kinatokana na sababu mbali mbali, miongoni mwa sababu hizo ni kama ifuatavyo:

(i) Kuachana kwa wanandoa,
(ii) Matumizi mabaya ya mitandao na simu,
(iii) Tamaa,
(iv) Watoto kukosa malezi mazuri,
(v) Kutofuatwa kikamilifu kwa Kanuni ya Nidhamu za Wanafunzi za mwaka 1996,
(vi) Kutokufuatwa kikamilifu Kanuni za Miiko na Maadili ya Kazi ya Ualimu za Mwaka 1995 na
(vii) Kutotumika ipasavyo Kanuni ya Adhabu ya Viboko ya Mwaka 1988.

Mhe. Naibu Spika, hizo ni miongoni mwa sababu ambazo zinapelekea masuala haya kutokea. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Ahsante sana, nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, na namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake. Mhe. Naibu Spika, ni jambo la kuleta matumaini kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imefanya huo utafiti kubainisha chanzo cha matokeo ya udhalilishaji katika skuli zetu.

Mhe. Naibu Spika, sasa tumeona sababu, lakini baada ya utafiti kawaida kunakuwa kuna *policy recommendation*, yaani mapendekezo ya kisera.

a) Naomba kumuuliza Mhe. Waziri. Nini kimetekelezwa baada ya kubainika vyanzo hivi vinavyosababisha udhalilishaji katika skuli zetu.

b) Mhe. Waziri alipokuwa anajibu alikuwa anafanya vile vile *reference* kwamba pamoja na mambo mengine, vyanzo vyengine ni kutokutumika kufuata kikamilifu kanuni ya nidhamu ya mwaka 1996. Mwaka 1996 ukihesabu sasa hivi ni *25 years* na nyengine ni miko na maadili ya kazi ya ualimu ya mwaka 1995 ni *26 years*. Lakini kutotumika ipasavyo kanuni ya adhabu na viboko ya mwaka 1988 ni miaka 33.

Mhe. Naibu Spika, namuuliza Mhe. Waziri, wanafanya nini kuona au kuhakikisha kwamba haya maeneo yanapitiwa yanafanyiwa *review*, ili kuleta muongozo bora wa hizi kanuni katika mwaka wetu huu wa 2021 ambapo udhalilishaji umekuwa ukienda juu badala ya kushuka chini. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi: (Kny: Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Dkt. Saada Mkuya kwa swali lake la nyongeza. Naomba nijibu kama ifuatavyo, kwanza naomba kuanza na swali (b).

b) Ni kweli hizi kanuni zetu kama nilivyozitaja hapa miaka ni mingi sana na kama yale malengo yalivyo ni kwamba sasa hivi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, tumekuwa tunaendelea na vikao vyetu vya wadau mbali mbali wa elimu, ili kuona ni namna gani ambavyo tunaweza kuiboresha elimu yetu kwa ujumla yake.

Kwa hivyo, katika hili basi na haya yote yanaingia katika miongoni mwao, baada ya hapo maana yake ni kwamba tutafanya mapitio ya kanuni na sera na mambo mengine yote ambayo yanahusiana na mfumo mzima wa elimu, ili kuona kwamba mustakabali mzuri wa elimu kwa vijana wetu unaelekea vizuri, lakini hata katika kulinda maadili ya vijana wetu wa Kizanzibari.

a) Vyanzo ambavyo tumevibainisha ni kwamba hivi zaidi vinagusa jamii kwa ujumla wake. Sisi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tunatoa elimu kwa jamii yetu kuhusiana na namna bora ya kuangalia kwamba wazazi kuachana na talaka zile ambazo hazina msingi, lakini vile vile katika kusimamia malezi mema na mazuri kwa vijana wetu, pia katika kutoa elimu na kuwaacha vijana wetu kama ambavyo nimeeleza kwamba matumizi mabaya ya mitandao na simu. Tunawakataza wanafunzi wetu kutotumia simu wakiwa katika maeneo ya skuli, kwani suala ambalo linashirikisha jamii kwa ujumla wake.

Kwa hivyo, ningeiomba sana jamii yetu tushirikiane kwa pamoja katika kuona kwamba, hivi visababu ambavyo vinapelekea matatizo haya kwa vijana wetu ya udhalilishaji, jamii kwa ujumla tunasimama kwa sauti moja kupiga vita na kuona kwamba matokeo haya yote yanakoma na yanaondoka kabisa. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa serikali imesema imefanya utafiti huo 2016. Mhe. Naibu Spika, naomba kuuliza na kutaka kujua kwamba

a) Je, utafiti huo ulifanywa na taasisi gani?
b) Utafiti huo hadi kumalizika kwake ulitumia kiasi gani?

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi: (Kny: Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir Mwakilishi wa Kundi la Vijana. Vijana Oyeee.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi: (Kny: Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba utafiti huu ulisimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, kwa sababu ndio ambayo inajukumu kubwa la kusimamia masuala yote ya tafiti katika wizara.

Kuhusu suala la bajeti, hili nitaomba nimletee kwa maandishi, kwa sababu kwa haraka haraka siwezi kujua ni shilingi ngapi. Lakini pesa ambazo zinatumika, zile fedha ambazo serikali inazipanga katika bajeti yake ya kila mwaka ambayo inakuwa inasimama, kuna fungu maalum kwa ajili ya kufanya tafiti. Lakini kiasi gani kilichotumika Mhe. Naibu Spika, hili nitaomba nililete kwa maandishi. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed:** Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba kumuuliza Mhe. Waziri maswali yangu mawili ya nyongeza. Mhe. Naibu Spika, tuliona mwanafunzi mmoja ambaye alifanyiwa udhalilishaji na mama yake mzazi na kumwagiwa mafuta ya moto na kumsababishia majeraha makubwa.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali,

a) Je, kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali mmetoa mchango gani ili kuhakikisha yule mama anapaata adhabu stahiki.
b) Kwa kuwa yule mtoto alikuwa katika kipindi cha mitihani na ikalazimika kufanya mtihani. Je, mitihani yake aliweza kufaulu vizuri. Naomba utueleze. Ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi: (Kny. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Napenda kumjibu Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed Mwakilishi wa Mkoa wa Magharibi kinamama Viti Maalum.

a) Mhe. Naibu Spika, ni kwamba mwanafunzi ambaye alipata jeraha kutokana na mama yake mzazi. Binafsi na sote tulimuona Mhe. Waziri alivyokuwa akifanya ziara ya kumtembelea yule mtoto mara kwa mara katika hospitali. Lakini sambamba na hilo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilihakikisha kwamba mtoto yule haki yake ya kufanya mtihani anaipata, na aliipata na mtoto yule alifanya mtihani.

Kwa hivyo, huo ni mchango mkubwa sana ambao serikali yetu imeutoa kwa kupitia kuona kwamba mtoto yule anaweza kupata haki yake ya msingi.

Mhe. Spika, suala la kuona kwamba sheria inatumika. Nadhani huu ni wajibu wetu, hata na sisi Baraza la Wawakilishi kazi yetu ni kusimamia sheria ambazo tunazitunga hapa. Kwa hivyo, ni wajibu wetu sasa kuhakikisha kwamba tunaona mama yule sheria inasimama na inachukua

mkondo wake katika kuona kwamba anaadhibiwa kwa mujibu wa sheria na kwa kosa ambalo amelifanya ili iwe ni funzo kwake na kwa wengine.

b) Kuhusiana na ufaulu wa yule mtoto. Kwa taarifa nilizosikia kwamba yule mtoto amefaulu, kwa sababu ametoka Darasa la Sita kuingia Kidato cha Kwanza. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

**Nam. 19**

**Changamoto ya Ukosefu wa Huduma za Umeme Katika Maeneo ya Vijiji Vya Mwanguo na Chanjaani**

**Mhe. Abdalla Abasi Wadi –** Aliuliza:-

Katika jimbo la Nungwi mpaka hivi sasa viko vijiji vichache kama vijiji vya Mwanguo na Chanjaani ambavyo bado huduma ya umeme haijafikishwa na wananchi wanapigia kelele ili kupata haki yao hii.

Je, wizara ina mpango gani kuwaletea huduma hii.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini -** Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 19 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme imefanikiwa kusambaza umeme kwa zaidi ya asilimia 90 katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Shirika la Umeme, ni kuhakikisha kwamba maeneo yote yaliyobaki yanasambaziwa huduma ya umeme ndani ya miaka mitano kuanzia sasa.

Mhe. Naibu Spika, vijiji vilivyobaki vitasambaziwa huduma ya umeme hatua kwa hatua hadi kukamilika. Hivyo, katika kijiji cha Mwanguo tayari Shirika la Umeme limeshaweka *transformer* katika eneo la Kidagoni, kazi iliyobakia ni usambazaji wa umeme mdogo wenye urefu wa kilomita mbili ambayo itakamilika ndani ya muda wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/2021.

Aidha, Mhe. Naibu Spika, kazi ya kupeleka umeme katika kijiji cha Chanjaani itaingizwa katika Bajeti ijayo ya mwaka wa Fedha 2021/2022. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Abdalla Abasi Wadi:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa serikali yetu ni sikivu sana na ni tendaji.

Je, ni lini usambazaji wa hizi nyaya ndogo za umeme katika kijiji hiki cha Mwanguo, hasa ukizingatia kwamba ni kilomita mbili tu ya nyaya zilizobakia. Ni lini tutasambaziwa umeme huu?

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, nimeeleza katika majibu yangu mama kwamba ndani ya kipindi hiki cha bajeti tutahakikisha kwamba kijiji cha Chanjaani kinasambaziwa umeme. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, tayari tuna *plan* ya vijiji mbali mbali ambavyo tunavisambazia umeme. Kwa hivyo, ndani ya bajeti hii tutahakikisha kwamba kijiji hiki umeme unafikishwa.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mhe. Waziri alipokuwa anajibu ameeleza kwamba sasa hivi tumefikia zaidi ya asilimia 90 katika usambazaji wa huduma za umeme vijijini. Naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na serikali yetu kwa jitihada hiyo kubwa ambayo inaendelea kufanyika katika kuwasambazia wananchi wetu huduma hii muhimu ya umeme. Lakini pamoja na pongezi hizo nilitaka kujua kwa kuwa Jimbo la Micheweni pia kuna vijiji vingi ambavyo bado havijafikiwa na umeme na maelezo ambayo yako mezani kwa wizara, ni kwamba wananchi hawa wanatakiwa wanunuwe nguzo za umeme ili waweze kusambaziwa umeme katika maeneo yao.

Mhe. Waziri nilitaka kujua je, una mpango wowote mwengine mbadala wa kuachana na kuwachangisha wananchi kununua nguzo za umeme na badala yake kuwasambazia hizo nguzo za umeme na wananchi wetu wakaweza kupata huduma kama vile ambavyo azma ya serikali yetu.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza lililoulizwa na Mhe. Shamata Shaame Khamis Mwakilishi wa Micheweni kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba hakuna mpango wa kuwanunulisha wanavijiji nguzo kwa ajili ya kufikisha huduma hii. Huduma ambayo itatozwa ada ni ile ya mtu mmoja mmoja.

**Mhe. Miraji Khamis Mussa:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri alisema kijiji cha Chanjaani mwaka huu katika utekelezaji kibajeti wanataka kupima ule uhalisia kama hili jambo kweli lipo.

a) Je, mmetenga kiasi gani cha fedha katika kusambaza umeme katika hiki kijiji cha Chanjaani katika swali la msingi.
b) Itakapokuwa tunaingia katika bajeti, taasisi yako ambayo iliahidi ndani ya Baraza hili haijatekeleza hili. Je, nini kauli ya serikali kwa wakati huo, watakuja kutuomba radhi au watakuja kusema wameihamisha katika mwaka ujao wa fedha.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba niombe kwanza kuhusiana na hili suala la fedha kiasi gani zilipangwa kwenye bajeti.

a) Mhe. Naibu Spika, naomba nilete jibu hilo kwa maandishi.
b) Mhe. Naibu Spika, nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba kabla ya bajeti kijiji hiki kitakuwa kimepata umeme na hatutokuja kuwa na sababu ya msingi ya kusema kwamba tumezi-*allocate* au kuzipeleka sehemu nyengine yoyote.

**Nam. 10**

**Matengenezo ya Meli ya MV. Maendeleo Chelezoni Mombasa**

**Mhe. Mussa Foum Mussa:**

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

*(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)*

**Nam. 37**

**Changamoto za Wavuvi Kutofahamu Utaratibu wa Kisheria**

**Mhe. Hassan Hamad Omar** – Aliuliza:-

Wavuvi wamekuwa wakisumbuliwa kisheria kwa kuvua uvuvi haramu.

(a) Je, upi uvuvi halali na haramu kwa mujibu wa sheria ya uvuvi ya Zanzibar.

(b) Je, serikali ina mpango gani wa kukaa na wavuvi na jumuiya za kijamii zinazo husika na uvuvi kuchambua sera na sheria za uvuvi wa kuelekea uchumi wa buluu.

(c) Je, utawaunganisha vipi wavuvi wadogo wadogo katika harakati za kuleta maendeleo na kuchangamkia fursa za uchumi wa buluu.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi –** Alijibu:-

Ahsante Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Hassan Hamad Omar Mwakilishi wa Jimbo la Kojani, naomba kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba Serikali ya Awamu ya Nane, chini ya uongozi wa Rais mpendwa na raia wake Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwamba haina nia wala haitokuwa na nia ya kuwasumbua wavuvi, badala yake ina nia ya kuwasaidia wavuvi wote wa Zanzibar.

Pia naomba kumkumbusha Mhe. Mwakilishi kwamba sheria ya uvuvi haramu imetungwa na Baraza lako tukufu, na hivyo ikiwa yako maeneo anayaona yana kingana na taratibu za uvuvi, basi taratibu zetu tulizojiwekea za kupendekeza mabadiliko hayo zinaeleweka.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 37 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, uvuvi halali ni uvuvi unaotumia zana au njia za uvuvi zinazokubalika kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi nam.7 ya mwaka 2010. Aidha, uvuvi haramu ni uvuvi

unaotumia zana au njia za uvuvi zinazokatazwa kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi nam.7 ya mwaka 2010. Kwa maana nyengine zana za kuvulia zinaweza kuwa halali lakini zikatumika kuvua kwa njia haramu.

Mfano, nyavu ya kuvulia dagaa ukaitumia kuvulia katika maeneo ya hifadhi au kuvua samaki wadogo wadogo, huo ni uvuvi haramu. Aidha, kwa mujibu wa sheria kuvua samaki wachanga, waliokuwa hawajafikia viwango, kutumia gesi kwa kuvulia, kutumia miwani (vioo) kwa kuvulia, na nyavu za kukota ni miongoni mwa uvuvi haramu.

(b) Mhe. Naibu Spika, wizara tayari imeanza na inaendelea kukaa na Jumuiya za Wavuvi, Kamati za Uvuvi na vikundi vyote vinavyojishughulisha na uvuvi, ufugaji na mazao ya baharini, wadau wanaojishughulisha na biashara ya mazao ya baharini na wakulima wa mwani, ili kuwafahamisha juu ya dhana nzima ya Uchumi wa buluu kwa ajili ya kupitia sera, sheria na kanuni zake.

Wizara yangu inaendelea kutoa elimu ya kuwafahamisha wavuvi na wadau wa Sekta ya Uvuvi namna ya kupata mitaji ya kundeleza biashara zao ili kutumia vyema fursa za Uchumi wa Buluu. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Suleiman Makame Ali ulisimama.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Mheshimiwa mpe mwenyewe mwenye suala la nyongeza.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Hassan Hamad Omar.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa kunijibu vizuri na kwa ufasaha kabisa. Lakini Mheshimiwa pamoja na yote hayo nina swali langu la nyongeza (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wavuvi wanatumia chupa ya gesi kwa ajili ya kupata pumzi katika utendaji wao wa kazi vile vile wavuvi wanatunia vioo kwa sababu ya kuona shughuli wanayoitenda pamoja na kujikinga na wanyama wakali wa baharini vile vile wanatumia viatu kwa kuwasaidia kuogelea Mhe. Naibu Spika, namuuliza Waziri kwa sababu hiyo kuna uharamu gani wanaotumia wavuvi ili ikawa kutumia chupa ya gesi na kutumia vioo kuna uharamu gani unaotumika Mheshimiwa.

b. Kwa sababu hiyo, kwa mlahaka huo ni nini sheria hii italetwa Barazani ili kufanyiwa marekebisho. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Hassan Hamad Omar maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

a. Mhe. Naibu Spika, suala la kutumia gesi, kutumia vioo, na kutumia mishale ni masuala ambayo tumekubaliana katika sheria kwamba haya ni mambo ambayo yanaathiri uvuvi. Sasa pale itakapothibitika kwamba utumiaji wa gesi na vioo hayaathiri hapo tutaangalia na tutazungumza na wahusika tutafanya marekebisho lakini mpaka tuthibitishe kwamba kweli haya hayaathiri uvuvi.

b. Swali la pili. Marekebisho nimesema katika jibu langu la awali kwamba marekebisho tuna taratibu zetu za kufanya marekebisho ya sheria zetu. Kwa hivyo, taratibu naomba Mhe. Mwakilishi afate taratibu zetu ili tufanye marekebisho hayo anayoyahisi yanahitajika. Ahsante Mheshimiwa.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Maryam Thani Juma, swali la pili la nyongeza.

**Mhe. Maryam Thani Juma :** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa vile Mhe. Naibu Spika, kwenye jibu mama ametwambia kwamba ipo sheria Nam.7 ya Uvuvi na tukiangalia kwamba tunataka tuelekee kwenye Uchumi wa Buluu.

Mhe. Naibu Spika, nimwambie kwamba kuna zile sehemu ambazo za hifadhi ya uvuvi moja wapo ni Fundo lakini kuna wavuvi ambao wanatokea maeneo ya Ndagoni na maeneo mengine wanavamia maeneo yale, je Wizara ina mpango gani wa kudhibiti watu kama hawa wakitokea kufanya hali kama hiyo?

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo;-

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni tumeanza kugawa boti za doria na nia yake ni kuhakiki na kupitia maeneo yote hayo. Kwa hivyo, hilo eneo ambalo bado linaendelea na uvuvi haram mimi nataka nikuhakikishie nalichukua na tutaanza kulishughulikia kwa ipasavyo nakushukuru.

**Mhe. Naibu Spika:** Swali la mwisho Mhe. Suleiman Makame Ali.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukru kwa kunipa, nafasi hii ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Waziri katika majibu yako umezungumzia suala la Miwani pamoja na chupa. Mhe. Waziri wavuvi wanaozamia kuvua jongoo wale barango, pauni, kijino, spinyu wanakuwa chini ya maji kina kikubwa kuanzia pima kumi na tano hadi ishirini na ni lazima wanapozamia waweze kuvaa miwani hiyo. Lakini sasa uharamu huu unakujaje wakati wale wanakwenda kule na wakuja na kitu ambacho kwamba ni sahihi kama pweza kilo kumi mpaka kumi na tano. Je, Mhe. Waziri huoni kwamba sasa ipo haja kuweka hii sheria kwamba wavuvi hawa uharamu wa kwenda kule na chupa uweze kuondoka kuona kwamba wavuvi hawa wananufaika na bahari. Lakini pia tunakwenda katika uchumi huu wa buluu.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifutavyo:-

Naomba nimbukushe Mhe. Mwakilishi kwamba suala la uvuvi wa majongoo kwa hiyo namna anayoieleza yeye ni haramu, majonjoo yanayoruhusiwa kuvuliwa ni yale majongoo ambayo yanafugwa peke yake. Kwa hivyo, uvuvi unaoueleza wewe ni haram kwa hivyo hatutoruhusu kuvua majonjoo hivyo namna ilivyoyaeleza. Nakushukuru Mheshimiwa.

**Mhe. Haji Omar Kheri :** Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali. Nimpongeze pia Mhe.Waziri kwa majibu mazuri ya maswali yote yaliyoulizwa na mimi naomba niulize swali la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo;-

a. Kwa kuwa sheria Nam. 7 ya mwaka 2010 bado ipo ambayo inadhibiti uvuvi haram na kwa kuwa wizara yake kupitia Idara ya Uvuvi imetunga kanuni mbali mbali zilizotajwa ndani ya sheria kuruhusu maeneo tengefu kama Minai, Hemkwa, Heka na Tumka na kwa kuwa maeneo hayo yote ni ya hifadhi ni kwanini Idara ya Uvuvi kupitia Wizara yake inaendelea kuruhusu uvuvi haram kufanyika katika maeneo hayo tengefu hususan katika eneo la Tumbatu kwa maana ya Hifadhi ya Tumka.

b. Hatua gani atazichukua Mhe. Waziri kuhakikisha kwamba uvuvi haramu kwa mujibu wa sheria kudhibiti vifaa hasa mishale katika kuzamia na kwenda kuvulia au kutafuta pweza au kupiga samaki wengine huku tukijua kwamba pweza anavuliwa kwa kumtoa kwenye pango yake kwa uchokoo na sio kupia mshale. Ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Haji Omar Kheri maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

a. Mhe. Naibu Spika, suala la ruhusa ya kuvua katika maeneo haram ruhusa hiyo haitolewi na Idara yangu nataka nikuhakikishie kwamba sisi tunafanya doria kuzuia uvuvi haram maeneo hayo. sasa ikiwa yanafanyika hao wanaofanya wanafanya kinyemela ni kama wezi kwa hivyo mimi wizara yangu au Idara yangu haifanyi au haitoi ruhusa ya kuvua katika maeneo hayo hilo la kwanza.

b. Suala la pweza kwamba ni lazima wavuliwe kwa kuchokoa na kubaliana nae tumesema yapo mambo ambayo huwa yanatumika Mheshimiwa ikiwa unatumia, pweza unaenda kumvua katika nyumba yake kwa mujibu wa taratibu zinazokubalika huo si uvuvi haram lakini ukiwa unatumia mshale huo huo kuharibu matumbawe huo ni uvuvi haramu inategemea namna gani zana hiyo unaitumia nakushukuru Mheshimiwa.

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa ahsante nakushukuru.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hotuba ya Uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi iliyotolewa tarehe 11/02/2020 na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Waheshimiwa Wajumbe majaliano kama alivyosema Katibu yanaendelea yaanyohusu hotuba ya Uzinduzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi iliyotolewa tarehe 11/02/2020 na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa

bahati Wajumbe  wa Baraza la Wawakilishi wengi wao wameshachangia ina maana waliobakia sasa kuchangia ni Waheshimiwa Mawaziri.

Kwa maana hiyo basi nina orodha hapa ya Waheshimiwa ambao watakuja kuchangia na kujenga baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wawakilishi. Sasa kwa maana hiyo, naomba sasa nimpishe Mhe. Mwenyekiti Mhe. Shaaban Ali Othman aweze kuendelea na shughuli yetu hii ya leo mpaka hapo mchana Mheshimiwa karibu sana.

*(Hapa Mhe.Mwenyekiti, Shaaban Ali Othman alikalia kiti)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe kama alivyokwisaha kueleza Mhe. Naibu Spika, Mjadala unaendelea na kwa mujibu wa orodha ya wachangiaji naomba sasa nimwite Mhe. Waziri waUtalii na Mambo ya Kale atafuatiwa na Mhe. Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Katibu, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ajiandae.

**Mhe. Waziri wa Utalii na Mabo ya Kale:** Ahsante sana, Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba na mimi kuchukua nafasi hii kuchangia hotuba ya Mhe. Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Uzinduzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi mnamo Novemba, 2020.

Kwanza kabisa hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ktuwezesha muda huu kuwa wazima wa afya na tukaendelea na majukumu kama Wawakilishi wa wananchi katika Chombo hiki kikubwa.

Lakini kwa nafasi ya pekee nichukue nafasi hii kumpongeza kwanza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar kwa kura nyingi hii inamaanisha imani kubwa ambayo wanayo wananchi zidi yake na kumuamini kuwa ni kiongozi ambaye anaweza kuongoza taifa letu.

Lakini pia, nimpongeze Mhe. Rais kwa uteuzi wake wa kumteua Makamu wa Pili na Makamu wa Kwanza wa Rais uteuzi ambao unaoonyesha imani yake na dhamira yake ya kuleta mabadiliko kwa Zanzibar. Pia ichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais kwa uteuzi wake wa Mwanasheria Mkuu pamoja na viongozi mbali mbali wakiwemo Mawaziri, Katibu Mkuu Kiongozi na Makatibu Wakuu mbali mbali ambao wameteuliwa katika Wizara mbali mbali.*(Makofi)*

Lakini kwa nafasi ya peke yake niwape hongera viongozi wote Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao wamechaguliwa katika majimbo na nafasi mbali mbali ikiwemo umoja wa Wanawake ambao umenifanya mimi hapa kusimama, kwa kweli nashukuru sana nawapa pongezi za dhati. *(makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa hotuba ya Mhe. Rais ukiisoma hotuba ambayo ameitoa naungana na wachangiaji wote ambao wamechangia, hotuba hii imekuwa ni dira na yenye maono ambayo inaturahisishia sisi watendaji wake kutekeleza majukumu yetu kwa urahisi na kwa wepesi zaidi kwa hiyo, nitoe pongezi  za dhati kwa Mhe. Rais kwa kutupa dira ya muelekeo

wa Serikali yake ya Awamu ya nane jinsi gani imejipanga katika kuhakikisha inapeleka mbele maendeleo ya uchumi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nichukue nafasi hii kuwapongeza Wajumbe wote ambao walichangia hotuba hii kwa nafasi ya kipekee ambao wamechangia katika Sekta yangu ya Utalii na kuorodhesha changamoto mbali mbali na kutoa ushauri mbali mbali, nataka niwathibitishie kuwa kama waziri mwenye dhamana ya Utalii, changamoto ambazo wamezileta hapa mbele ya Baraza lako tumezisikia kwa ajili ya utekelezaji na yale mashauri yote ambayo wametupa tutajitahidi kwa uwezo wetu kukuhakisha tunayafanyia kazi.

Nikienda moja kwa moja katika kuchangia hotuba ya Mhe. Rais, Mhe. Mwenyekiti, katika Wizara yetu ya Utalii ambayo tunasema ni Wizara mama ambayo inachangia takriban asilimia 28 ya *GDP* lakini pia tunategemea kuwa asilimia 28 ya *foreign exchange* tumejipanga na mikakati ifuatayo kukabiliana na changamoto mbali mbali lakini pia kuendeleza Sekta ya Utalii kama ifuatavyo:-

1. Tumepanga katika miaka hii mitano katika wizara yetu kuhakikisha kuwa tunaibua masoko mapya ya utalii na kujitangaza zaidi duniani. Tunajua Zanzibar inajulikana duniani kote kama ni eneo la utalii tunasema ni *tourist destination all of the world*, lakini bado tunahitaji kujitangaza zaidi kwa kutumia mbinu mbali mbali na za kisasa zaidi kwa ajili ya kujitangaza zaidi na kujulikana vivutio vyetu mbali mbali ambavyo vimo.

Tunajua Zanzibar soko letu la utalii limekuwa ni Ulaya ya Magharibi kwa kipindi kirefu kabla ya kuja kwa Mripuko wa maradhi wa *COVID 19* lakini kwa kipindi hiki tumekuwa na soko jipya la utalii ambalo ni Ulaya ya Magharibi zikiwemo nchi za Poland pamoja na Czech na nchi nyengine za Ulaya Mashariki ambazo kwa sasa ndio wageni wengi ambao wanaingia.

Kwa hivyo, wizara tumejipanga kuhakikisha kuwa kwanza tunali-*maintain* soko ambalo tunalo ambalo ni soko jipya lakini pia na soko letu ambalo lipo kwenye kipindi cha athari ya maradhi ya *COVID 19* tunaendelea kushikilia na kuwasiliana nao kwa karibu ili kuhakikisha kuwa maradhi yatakapo kwisha soko letu linarudia katika hali yake ya kawaida.

2. Tumejiopanga kulinda kuhifadhi na kuongeza ubora wa vivutio vyetu mbali mbali vya utalii pamoja mila na desturi za kizanzibar. Hili ni eneo muhimu tunapozungumza Zanzibar utalii tunao wa kimazingira ambao unajulikana uko utajiri katika maeneo ya fukwe katika maeneo ya bahari na maeneo ya viungo.

Lakini pia kuna kipengele cha utamaduni ambacho ni muhimu sana na kina tunzwa sana duniani kama ni kivutio kwa ajili ya utalii wetu. Kwa hiyo, kama wizara tutahakikisha tunasimamia kuulinda na kuuhifadhi utamaduni wetu lakini na kulinda na kuhifadhi maeneo yetu ya kihistoria likiwemo eneo la Mji Mkongwe ambalo ni kivutio kikubwa kwa watalii kutoka sehemu mbali mbali duniani.

Tukizingatia kuwa Mji Mkongwe ni sehemu ya urithi wa dunia, kwa hiyo kama serikali tutashirikiana na wawekezaji binafsi kuhakikisha kuwa Mji Mkongwe unakuwa unatumika zaidi katika shughuli za kitalii ili kuingiza zaidi pato katika nchi yetu na isiwe kama ulivyo sasa kuwa

mara nyingi unakuwa na changamoto za Mji kuwa na mazingira hatarishi na majengo ambayo ni hatarishi kwa usalama wa raia wetu.

Lakini pia kama Wizara tunahakikisha tunafikia malengo ya utalii kama ilivyoelezwa katika hotuba tutahakikisha tunaanzisha vivutio vipya vya utalii Unguja na Pemba. Vivutio hivi tutavianzisha kulingana na uwezo utakavyo ruhusu tukishirikiana pamoja na Sekta Binafsi. Vivutio hivi vikiwemo kama vile tunatarajia kuanzisha au kuwekeza kutafuta wawekezaji kuekeza katika kumbi za mikutano ya kimataifa *Amusement Park*, *Water Sport*, *Sport Complex Centre*, maduka makubwa ya kisasa ya kitalii *Opera House*, *Animal Park*, utalii wa visiwa vidogo vidogo, ujenzi na makumbusho mpya ya kisasa. Hivi ni katika maeneo ambayo tumeyasema katika kipindi hichi cha miaka mitano tuweze kuwekeza nguvu zetu huko tukishirikiana na sekta binafsi ili kuhakikisha kwanza tunatoa nafasi za ajira, lakini pia tunaongeza idadi ya watalii kutembelea na pia kuongeza kipato kwa ajili ya nchi yetu.

Nne, pia tumepanga kama Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale katika kuhakikisha tunafikia malengo na dira ya Hotuba ya Mhe. Rais, tumehakikisha kujipanga tunadhibiti ukusanyaji wa mapato pamoja na kodi katika Sekta ya Utalii katika bidhaa mbali mbali za utalii ambazo tunazo. Kwa hiyo, kuhakikisha huko kwanza tumejipanga kuhakikisha tunabadilisha mfumo wa kukusanya mapato kutoka mfumo wa kawaida au wa *cash* na kwenda kwenye *electronic*, ambapo malipo yote yatafanyika katika mfumo wa *electronic online* ikiwemo katika kusajili leseni za biashara mbali mbali za utalii. Ndani miaka mitano hii, tutahakikisha kuwa malipo yote yanafanywa *online* na usajili wa leseni zote za biashara zote za utalii zinafanywa ki-*electronic* ili kuhakikisha mapato yote na kuzuia ile mianya ambayo ipo.

Pia, katika kuhakikisha tunadhibiti ukusanyaji wa Mapato katika Wizara, katika Sekta ya Utalii tumeanzisha mfumo rasmi wa kupanga madaraja ya hoteli kupitia *electronic* na kuacha mpango wa sasa ambao unakuwa muombaji anajaza fomu tu akiwa yupo *manually* bila ya udhibiti wowote. Kwa hivyo, tutaweka mfumo ambao muombaji anayeomba kufanyiwa hoteli yake ni daraja gani ambao utakuwa *automatic unam-cancel* akiongeza tu zile sifa kwamba zinamueka kwamba kwa sifa hizi au huduma hizi ambazo unazo kwenye hoteli yako, kwa hiyo itakua ni daraja la kwanza, daraja la pili au daraja la tatu. Kwa hiyo, hichi ndio kitu tumejipanga katika kuhakikisha kuwa pato la Sekta ya Utalii na Kodi kwenye Sekta ya Utalii zinapatikana kama inavyohitajika.

Mhe. Mwenyekiti, katika kupambana na changamoto ya *Covid 19* kama Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, tumepanga kuendelea kusimamia *standard operating protocols* ambazo zipo katika wizara na ambazo zinatakiwa kutumiwa katika maeneo yote ambayo wageni wanaingia kwa ajili ya kuzuia maambukizi mapya ya maradhi ya *Covid* na kufuata masharti yote. Katika *standard operating protocols* zimeeleza hatua mbali mbali ambazo zinatakiwa kufuatwa tangu mgeni anaingia *airport* lakini wakati anapopokelewa katika hoteli, anapokuwa katika gari ya kutembeza wageni lakini pia anapokuwa na yule mtembezaji wa watalii vitu gani anatakiwa avifate kwa ajili ya usalama wa afya yake lakini pia kwa ajili ya usalama wa wananchi wetu ambao wapo katika maeneo mbali mbali.

Kwa hivyo, kama wizara tutahakikisha tunalisimamia hili kwa vile dunia yote kipindi hichi ipo katika janga hili. Lakini pia kwa vile wageni tumeshafungua na wanaendelea kuingia ni nafasi ya kujikinga na changamoto na maambukizi zaidi kwa wageni na kwa wazawa ambao tupo tunahudumia watalii.

Mhe. Mwenyekiti, pia tumejipanga kuongeza idadi ya watalii katika nchi yetu lakini pia na kuongeza siku za kubaki katika nchi yetu. Hili kama wizara tumejipanga kwa kuhakikisha kuwa vivutio vyetu ambavyo tupo navyo, tunaviongezea ubora wake na kumpa fursa zaidi mtalii baada ya kuishia tu kwenye fukwe lakini awe na sehemu za kutembelea pengine katika misitu, au kwenye mashamba ya viungo, au sehemu wanakuja kwa ajili ya ...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, hitimisha.

**Mhe. Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:** Naam

**Mhe. Mwenyekiti:** Hitimisha.

**Mhe. Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru lakini pia katika kuendeleza Sera ya Utalii kwa wote, kama wizara tutahakikisha kusimamia Sekta ya Utalii kwa wote na kuhakikisha kila mzawa wa nchi hii anafaidika na vyanzo vyote ambavyo vipo katika maeneo yao na wanashiriki moja kwa moja katika kuhakikisha kuvilinda na kuvitunza na kupata faida *direct benefit* ya ajira, katika vile vyanzo ambavyo vipo katika maeneo husika kwa ajili ya kuboresha usalama wa utalii na wananchi katika maeneo hayo wasijihisi kuwa ni utalii kwa ajili ya watu fulani lakini sote kila mmoja ajihisi amenufaika katika Sekta ya Utalii.

Mhe. Mwenyekiti, Naunga mkono hotuba ya Mhe. Rais kwa asilimia mia. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe nimeombwa hapa nimruhusu Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi baada ya yule niliyemtaja awali. Kwa hiyo, baada ya Mhe. Waziri, Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na ajiandae.

**Mhe. Waziri Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Mwenyekiti, naomba na mimi nikushukuru kwa kunipa fursa ya kuichangia Hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Uzinduzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema kuwepo hivi sasa kuwa tunaichangia katika hotuba ya Mhe. Rais. Pia nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa ushindi mkubwa alioupata. Hii ni ishara tosha kuwa wananchi wa Zanzibar wanamkubali vya kutosha. Pia nichukue fursa hii kumpongeza Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Hemed Suleiman Abdulla kuwa Makamu wa Pili wa Rais. Pia niwapongeze Wawakilishi wote walioteuliwa katika majimbo yao na wale wa Viti Maalum nikiwemo mimi mwenyewe. Mungu atuujaalie tuweze kuifanya kazi hii vizuri kabisa ili mwakani turudi tena *(Makofi)*

Pia, niichukue fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote tulioteuliwa na Mhe. Rais. Mungu atujaalie atupe uwezo wa kutekeleza majukumu yetu ambayo tumepangiwa na Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, sasa na mimi naomba kuichangia Hotuba hii ya Mhe. Rais, ambayo imeonesha matumaini makubwa kwa wananchi wa Zanzibar na kama walivyosema wajumbe wenzangu wengi hapa kuwa hotuba hii unaweza kutunga vitabu hata kumi endapo utaichambua. Kama tunavyoona kuwa hotuba imechukua kila kitu na imekua ni dira na muongozo kwetu sisi mawaziri ambayo itatusaidia katika majukumu yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu, mambo yote yaliyotajwa kwenye hotuba hii yaweze kutekelezeka vyema ili wananchi wa Zanzibar wapate maendeleo endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba hii naomba moja moja niende katika Uk. 14 ambao Mhe. Rais amelitaja suala la Bandari kwa kusema kuwa serikali ya Awamu ya Nane ina malengo ya kujenga bandari kubwa katika maeneo ya Mangapwani. Bandari hiyo ya kisasa itakuwa kubwa yenye sehemu kadhaa za kutolea huduma zikiwemo sehemu za kuhudumia meli zitakazobeba mafuta na gesi. Chelezo kwa ajili matengenezo ya meli, eneo la kuhudumia meli za kubebea mizigo na makontena, bandari ya uvuvi na bandari ya meli za kitalii. Mwisho wa kunukuu.

Kwa kweli, mwenye macho haambiwi tizama. Tumeshuhudia utiaji wa saini wa hati ya maelewano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mamlaka ya Uwekezaji wa Oman. Utiaji wa saini huu ulifanyika tarehe 28 Januari, 2021 ikiwa ni ndani ya siku 100 za uongozi wa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Hatua hii ya utiaji wa saini imedhihirisha wazi kuwa yajayo ni neema tupu, kwani mapato yataongezeka kwa kiwango kikubwa sana na ajira nyingi zitazaliwa endapo bandari ile tayari imeshajengwa na inaendelea kufanya kazi. Mpango huu kwa mujibu wa makubaliano utamalizika baada ya miezi sita ila kwa shauku tuliyonayo, tunaomba ikamilike kabla ya hapo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa mpango huu, serikali itafungua milango ya kuwashirikisha na kuwakaribisha wawekezaji mbali mbali kuja kuwekeza katika ujenzi wa bandari hizo ikiwemo ujenzi wa viwanda. Vile vile, Muonekano wa Mangapwani na Bumbwini utabadilika kabisa kutokana na ujenzi wa kisasa utakaojengwa pale. Wizara yangu ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi itasimamia kwa karibu katika utekelezaji wa makubalino hayo ili mpango huu ukamilike kwa wakati au kabla ya hapo na kwa kuwa hatua iliyokuwepo hivi sasa timu ya wataalamu imeshaanza vikao vyake. Waatalamu hao ni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wataalamu kutoka Mamlaka ya Uwekezaji wa Oman na vikao hivi ni mwanzo wa utekelezaji wa mpango huu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niende moja kwa moja kwenye suala la barabara ambayo imetajwa kwenye uk.19. barabara hizo zitajengwa kwa kiwango cha lami zenye urefu wa zaidi kilomita 197.6 kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashahidi hapa, katika vikao tulivyokaa, tumewasikia Wajumbe wengi waliochangia wamegusia suala la barabara kutokana na umuhimu wake. Zaidi wa asilimia 94 ya wajumbe wamechangia masuala ya barabara kwani barabara hurahisisha mawasiliano baina ya mji na vijiji na maeneo mbali mbali. Pia hurahisisha mawasiliano katika shughuli zetu

za kila siku ikiwepo shughuli mbali mbali za kijamii, biashara na Utalii. Hivyo, uchumi huimarika kupitia barabara hizi, hivyo kuwa na barabara mbovu inapelekea usumbufu mkubwa kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa ujenzi wa barabara, wizara tayari imeshaandaa mpango kazi wa miaka mitano kulingana na mahitaji ya barabara hizo, kama tunavyojua kwamba barabara ina gharama kubwa sana. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutafuta mikopo nafuu kuipitia mashirika yanayotoa mikopo hiyo ikiwemo *ADB. World Bank, Saudi Fund* na wengineo kwa lengo la kutekeleza mpango huu.

Serikali ina nia ya dhati kwa wananchi wake katika kuzijenga barabara na inatamani barabara hizo zijengwe ndani ya miaka mitatu. Ila changamoto kubwa ni uwezo mdogo kwani kwa mujibu wa wataalamu kilomita 1 ya barabara hujengwa kwa kiasi ya shilingi bilioni1.2 mpaka bilioni 1.6 za kitanzania. Hii hutegemea ha hali ya eneo ilipojengwa barabara hiyo. Kutokana na gharama hizo ndipo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inatafuta mbinu mbali mbali za kutafuta fedha kwa ajili wa ujenzi wa barabara. Huo ni kwa upande wa ujenzi wa barabara.

Mhe. Mhe. Mwenyekiti, Wizara pia inaendelea na zoezi la uzibaji wa viraka. Pia tumeona wachangiaji wengi wamesema kwamba barabara zao zina mashimo na wataendelea kuchangia. Kwa hivyo, wizara inaendelea kuziba hivyo viraka ila tumepanga tu tuende kwa maeneo. Tunatoka mjini na baadae tutaingia sehemu nyengine na zoezi hili ni endelevu na la kila siku.

Kama tunavyojua kwamba barabara nyingi zilizokuwepo ni za muda mrefu hasa katika maeneo ya mjini na imekuwa ni kero kubwa kwa watuamiaji wa barabara hizo. Hivyo, wizara imeamua kuchukua hatua za kuzifanyia matengenezo barabara ili ziweze kupitika kutokana na kuharibika vibaya. Wataalamu wanatueleza kwamba maisha ya barabara ni kwa muda wa miaka mitano, ikipita hapo barabara ile inatakiwa iparwe, itiwe barabara nyengine ambalo pia tunajua ni gharama kubwa kama nilivyosema hapo mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Viwanja vya Ndege ambavyo vimezungumzwa katika Uk.18 katika hotuba hii. Kama tunavyojua kuwa Viwanja vya Ndege ni sehemu muhimu katika kuongeza mapato. Kwa sasa kupitia Wizara yangu imeelekeza macho yake katika viwanja vya Ndege vya Abeid Amani Karume hasa kutokana na hatua za kukamilika kwa jengo jipya la *Terminal 3,* ambapo kukamilika kwake kutawezesha kuimarika kwa huduma zinazotolewa viwanjani hapo, jambo ambalo litapelekea ndege nyingi kubwa kutua hapo kutoka nchi mbali mbali. Katika uwanja wa Ndege, tunategemea pia mapato yataongezeka kutokana na watalii wengi ambao watakua wanakuja kutoka nchi mbali mbali. Kwa hatua hii, wizara inafuatilia kwa ukaribu zaidi ili kuhakikisha jengo hilo linamalizika na kukabidhiwa serikalini hivi karibuni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia katika kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais naomba nielekee Uk. 35, ambao umeeleza amani na utulivu. Mhe. Rais, ameliona jambo hili ni muhimu sana kwa taifa letu kwani bila ya amani na utulivu hakuna hata mpango mmoja ambao utakaotekelezeka.

Mwisho, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru ndugu jamaa na marafiki kwa ushirikiano wao mkubwa walionipa wakati wa harakati mbali mbali za uchaguzi uliopita. Nawashukuru sana kwa

dhati kabisa kina mama wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa kunipa kura nyingi na hatimae kufikia hadi leo, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti baada ya kuchangia mchango hua nasema kwamba naunga mkono hotuba ya Mhe. Rais asilimia mia Moja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, maombi yamekuwa mengi lakini sasa naomba nimuite mchangiaji anaefuta. Mhe. Waziri wa Ardhi, na Maendeleo ya Makaazi, atafuatiwa na Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo na Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utawala Bora ajiandae.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nianze kwa kukushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyeitoa katika Baraza lake la Kumi tarehe 11 Novemba, 2020.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyetujaalia uzima na afya njema sote tukiwa wazima na wenye afya. Lakini vile vile tuendelee kuwaombea wenzetu ambao ni wagonjwa, Mwenyezi Mungu awajaalie afya njema na wale ambao wameshafika mbele za haki *Allah Inshaallah* awajaalie, awasamehe makosa yao na awajaalie wawe miongoni mwa waja wake wema na sisi pia waja wake atujaalie mwisho mwema.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba niungane na wenzangu wote ambao wameendelea kuchangia katika hotuba ya Mhe. Rais wetu mpendwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Katika hotuba hii nilikuwa naomba na mimi nitoe mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuchangia kwangu naomba niinukuu hotuba ya Mhe. Rais katika Uk.7 inasema:-

"Tunapotaka kwenda na namna ambavyo sisi katika serikali tumejipanga, kutafsiri na kutekeleza Ilani ya CCM 2020-2025, ambayo Chama cha Mapinduzi kinachounda Serikali kimetuelekeza tuielekeze."

Sambamba na hili naomba nikariri vile vile hotuba ya Mhe. Rais katika Uk.8 anasema kwamba:-

"Hii kwangu ina maana kubwa sana nayo ni kuyatafsiri upya Mapinduzi yetu Matukufu na Muungano wetu katika kizazi kipya."

Tafsiri hiyo si nyengine bali ni kujenga Zanzibar mpya kwa kufanya mapinduzi mapya ambayo ni mapinduzi ya kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba kuzungumzia zaidi hapa, Mhe. Rais katika hotuba yake alielekeza kwamba tutaenda katika utekelezaji wa Serikali yetu hii ya Awamu ya Nane kama ilivyo taratibu za serikali kwa kufuata Ilani ya Chama ya Chama chetu ambavyo inasema lakini vile vile ahadi ambazo Mhe. Rais wetu alizitoa wakati wa kutafuta kura.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tunataka kuleta uchumi mpya. Uchumi kwa maana, tafsiri ya Mapinduzi mapya kwa maana ya uchumi mpya. Uchumi ambao kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, lengo la Serikali yetu ya Awamu ya Nane ni kuhakikisha kwamba tunapanga mji wetu katika utaratibu ulio mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, ni dhahiri Waheshimiwa Wawakilishi katika vikao mbali mbali wamechangia namna ambavyo nchi yetu imejengwa ovyo. Kuna baadhi ya mitaa ukienda kama kunatokea dharura basi ni shida kupitisha hata gari la kuzima moto. Hii ni kutokana na kwamba watu wamevamia miji na kujenga ndivyo sivyo. Kwa hivyo, katika kuona kwa Mapinduzi haya mapya ya kiuchumi yanakwenda vizuri na katika kuona kwamba Mapinduzi yetu matukufu na Muungano wetu tunaudumisha vizuri basi tutahakikisha kwamba tunapanga vizuri ardhi yetu ya Zanzibar na katika kupanga huko tutasimamia vyema ugawaji wa ardhi kwa mambo mbali mbali, ikiwemo makaazi ya wananchi sambamba na uwekezaji ambao tunataka kuufanya katika nchi yetu na uwekezaji katika nyanja zote viwanda, masuala ya mahoteli na kila aina ya uwekezaji.

Vile vile, kwenye makaazi tutahakikisha kwamba tunaweka utaratibu mzuri, kuona kwamba kila ambae anajenga na kwa baadhi ya mitaa fulani kwamba lazima kuwe na ujengaji ambao unaendana na hali na hadhi ya hiyo mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Serikali yetu ya Awamu ya Nane kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi tumejipanga katika kuhakikisha kwamba tunayatizama vyema maeneo yote tulioyatoa kwa ajili ya uwekezaji na kwa bahati mbaya sana maeneo haya hayajaendelezwa. Ni kwamba tunasema tunaendelea kupanga ardhi yetu vizuri, ili tupange ardhi vizuri ina maana itumike vizuri. Kuna baadhi ya watu walipewa maeneo kwa ajili ya kuwekeza, bahati mbaya sana maeneo haya yamekaa tu *idol* hayajafanywa chochote. Kwa hivyo serikali yetu itahakikisha kwamba maeneo haya inayarudisha serikalini kwa kuona kwamba wale ambao walipewa maeneo haya wameshindwa kuyaendeleza. Lakini vile vile kuna wale ambao walipewa maeneo makubwa sana kitu ambacho uwekezaji wao hauhitaji maeneo makubwa kiasi kama hicho. Mhe. Mwenyekiti, vile vile kwa maeneo hayo nayo serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ina nia ya kuona inarudi serikalini ili wapewe watu wengine na wao waweze kuyaendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile ningeomba kuzungumzia suala ambalo linahusiana na kuweka akiba ya ardhi ya Zanzibar. Tunataka kuendeleza nchi yetu kiuchumi ili uchumi mpya, ajira nyingi zipatikane lakini wawekezaji wengi zaidi waje katika nchi yetu. Ili kuona hili linafanikiwa, basi serikali imejipanga katika kuona kwamba inahifadhi ardhi yake kwa maana na kuwa na ile *land banking* ya ardhi ambayo itahifadhiwa vizuri na kupitia Serikali ya Mikoa na Wilaya basi tutahakikisha kwamba tunashirikiana kwa pamoja kuona kwamba ardhi hizi tunazilinda na zisivamiwe na mwananchi wa aina yeyote.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo wizara imejipanga katika serikali yetu hii ya awamu ya nane ni kuhakikisha kwamba tunajenga miji mipya ya kisasa. Miji ambayo itakuwa ina mambo yote mazuri, maana wenyewe wataalamu wanaita kama ni *Satellite City*. Hizi tutahakikisha kwamba tunazijenga katika mji wetu wa Zanzibar katika maeneo mbalimbali.

Vvile vile kuwa na makaazi ya bei nafuu na tutajenga miji mipya ili kuvutia wananchi wa ndani na hata wa nje, lakini vile vile kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanaendelea kuwa na

makaazi yaliyo bora. Kwa hiyo katika hili kuona linafanikiwa vizuri, wizara yetu imejipanga katika kuona tunajenga nyumba za kisasa za bei nafuu ambazo zitaweza kuwarahisishia maisha wananchi wa Zanzibar kati ya wale ambao wana kipato cha chini basi na yeye anaweza kumudu au kukodi au kununua nyumba za aina kama hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika serikali yetu hii ya awamu ya nane kama tunavyoelewa Mhe. Rais wetu katika hotuba yake na katika hotuba zake mbali mbali alikuwa anazungumza kwamba tuendelee kudumisha umoja wa wananchi wetu lakini tuhakikishe kwamba wananchi wetu wanapata kile ambacho wanastahiki. Kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi tutaendelea kutatua migogoro ya ardhi ambayo ipo kwa asilimia kubwa ndani ya nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, tunajiona dhahiri kwamba kuna migogoro mingi ya ardhi ambayo inasababisha na inatokana na sababu mbali mbali. Miongoni mwa sababu hizi kuna baadhi ya viongozi ambao wanasababisha migogoro, kuna wananchi kwa wananchi na mambo mengine ya kimazingira ambayo yanapelekea kuibuka kwa migogoro hii. Serikali yetu ya awamu ya nane itahakikisha kwamba migogoro hii tunaipatia ufumbuzi na kila ambae alikuwa anapaswa kuwa na haki hiyo basi anarejeshewa haki yake na yule ambae alidhulumu haki yaw engine basi na yeye anaacha haki hiyo na inarudi kwa mwengine ambae anapaswa kuwa na haki kama hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hayo naomba nitowe shukurani zangu za dhati kabisa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuniamini na kuniteuwa katika wizara hii na napenda sana nimuombe Mwenyezi Mungu anisaidie niweze kusimama imara, vile vile nawaomba viongozi wenzangu wote tushirikiane katika kuona kwamba tunaendelea kusimamia serikali yetu vyema na kwamba sote kwa umoja wetu tunaleta yale ambayo yajao ni neema tu na ambayo yanafurahisha.

Mhe. Mwenyekiti, nipende sana kumshukuru Mhe. Rais kwa uteuzi wake kwa Makamu wa Kwanza pamoja na jembe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Naamini kwamba uteuzi wake huu haukufanya makosa na naamini aliteuwa hakubahatisha hongera Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais. Vile vile nimpongeze kwa uteuzi wake wa kumchagua Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali jembe kijana kuliko wote naamini kwamba kwa timu ambayo Mhe. Rais ameiunda basi kwa uwezo wake *Allah* tutasimama sote imara.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kushukuru sana familia yangu yote kwa malezi mazuri ambayo wazee wamenipatia nawashukuru sana baba na mama yangu nawashukuru sana lakini vile vile namshukuru sana mume wangu mpendwa pamoja na watoto wangu kwa uvumilivu wao mkubwa katika harakati hizi ambazo kwa kweli muda mwingi nimekuwa nawanyima kwao lakini nawashukuru kwa ustahamilivu wao. Vile vile nikushukuru sana chama changu Chama cha Mapinduzi nakishukuru sana chama changu kwa kunisimamia katika kuona kwamba nasimama imara kuona kwamba ilani ya chama chetu tunaitimiza na kuisimamia ipasavyo. Nakishukuru sana chama changu katika Mkoa wa Kaskazini Unguja ngazi ya Mkoa, Wilaya, majimbo yote kwa ngazi zote, vile vile napenda sana kushukuru Umoja wa kina Mama wa Chama cha Mapinduzi kuanzia ngazi ya Taifa, Wilaya hadi Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa mashirikiano yao makubwa ambayo yamenipatia na naomba kuwaahidi kuwa sitawaangusha na naomba tuendelee kushirikiana.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante, sasa nimuite Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo atafuatiwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ ajiandae.

**Mhe. Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi niwe miongozi mwa wajumbe watakaoweza kuchangia hotuba hii nzuri ya Mhe. Rais. Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane kwanza na wengine kumshukuru Mwneyezi Mungu ambae ametujaalia tumeweza kufika hapa, lakini vile vile mimi pia nichukuwe fursa hii kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kunichagua mimi Tabia Mwita kuwa mwakilishi lakini vile vile kwa kunichagua kuwa waziri ninaehusika na masuala ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile naomba kuchua fursa hii kuwashukuru sana Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi. Kauli mbiu yetu inazungumza kwamba, “Umoja wa vijana ni tanuri la kuoka viongozi” mimi naamini ni miongoni mwa viongozi ambao wameokwa na wanaoendelea kuokwa, wanaoendelea kujifunza hadi Mhe. Rais Dkt.Hussein Ali Hassan Mwinyi akaweza kuona kwamba ninafaa kuwa miongoni mwa watu watakaoweza kumsaidia katika kuendeleza gurudumu la Awamu hii ya Nane kwa hivyo bila ya Umoja wa Vijana naamini kwa kiasi fulani pengine nisingeweza kuonesha mchango wangu katika nchi yetu. Nawashukuru sana Umoja wa Vijana na nachukua fursa hii kuwaahidi kwamba nitaendeleza mashirikiano ya dhati kwa umoja wa vijana wa Chama cha Mapinduzi lakini vile vile kwa Chama changu Cha Mapinduzi ambacho ndio mlezi wa Jumuiya hiyo kuhakikisha kwamba tunatekeleza vyema ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa pia nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais kwa uteuzi wake alioufanya kwa viongozi wetu mahiri ambao wanaendelea kusifiwa siku hadi siku tukianzia na Makamu wa Kwanza wa Rais, lakini vile vile Makamu wetu wa Pili wa Rais ambae ni kijana kabisa mchapakazi sote tunaona bidii na juhudi zake, lakini vile vile tunaona kabisa uzalendo wake namna anavyosimamia vyema shughuli za serikali na mimi kwa niaba ya familia yangu kwa niaba ya chama changu nasema naomba nimpongeze Mhe. Hemed Suleiman kumwambia tunamshukuru na tutamuunga mkono yeye na Mhe. Rais kuhakikisha tunamsaidia katika kuleta maendeleo.

Vile vile nachukuwa fursa hii kumpongeza sana kaka yangu na mwalimu wangu Dkt. Mwinyi Talib kwa kuchaguliwa kuwa Mwanasheria Mkuu ambae atatusimamia na kutusaidia kwenye masuala yote ya kisheria ili tuweze kuhakikisha nchi yetu inakwenda kwa utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa Katiba yetu ya Zanzibar ya mwaka 1984 na sheria zake zote zilizowekwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichangie hotuba ya Mhe. Rais kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba nianzie kwenye ukurasa wa 21 alivyozungumzia suala la matumzi bora ya sayansi na teknolojia. Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala la matumizi bora ya sayanasi na

teknolojia mimi nataka niseme kwamba Wizara yetu ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imejipanga vizuri juu ya matumizi haya bora kuhakikisha moja kwa moja vijana wanakuwa ndio wafaidika wakuu kwenye matumizi haya ya sayansi na teknolojia, pale ambapo tutakapoweza kuendeleza ile sera yetu ya viwanda kuhakikisha kwamba vijana wanakuwa na nguvu kubwa ya matumizi haya, ili waweze kuendesha viwanda na vile vile waweze kupata ajira kwa wingi kwa sababu tunafahamu kwamba vijana ndio nguvu kazi ya taifa na ndio wadau pekee ambao wanaweza kutusaidia katika masuala mazima ya viwanda.

Vile vile kwa kumuunga mkono Mhe. Rais ibara ya 163 ya ilani ya uchaguzi 2020 – 2025 pia imeonesha lengo nia na madhumuni hasa ya matumizi bora ya teknolojia na imemgusa kijana kama ndio mtumizi mkuu wa masuala ya teknolojia. Hivyo wizara yangu itahakikisha inasimamia vyema suala zima la kujipanga kutoa mafunzo kwa vijana wetu kuhakikisha wanaitumia vizuri hii sayansi na teknolojia.

Mhe. Mwenyekiti, ukienda katika ukurasa wa 29 Mhe. Rais alizungumzia sana suala zima la utawala bora na utawala bora huu ameuzungumza kwa upana wake na mimi niseme kwamba kupitia wizara yetu ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo tumejipanga vyema kushughulikia suala la Utawala Bora. Tunafahamu Utawala Bora una mambo mengi ikiwemo nidhamu serikali, uchapaji kazi, lakini ikiwemo suala zima la kufata Katiba na Kanuni zilizowekwa katika sehemu husika ili tuweze kwenda kwa mujibu wa utaratibu. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwaahidi wajumbe kwamba wizara yangu pia itakuwa na msimamo thabiti wa kuhakikisha unasimamia utawala bora kwa kusimamia nidhamu za wafanyakazi lakini vile vile kuchukua hatua kwa watendaji wowote watakaofanya uzembe kwa kupoteza mali za umma lakini vile vile kwa kuzorotesha maendelea ya wananchi na kuhakikisha nidhamu inapatikana.

Kwa hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa tushirikiane lakini naomba Waheshimiwa na ndugu wananchi tuvumiliane hakuna kitu kigumu kama kuleta mabadiliko. Tunajitahidi kumsaidia Mhe. Rais kuboresha Utawala Bora kwa sababu tunaamini ndio msingi pekee wa kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi. Mhe. Mwenyekiti, ukienda katika ukurasa wa 32 Mhe. Rais amezungumzia pia kwenye suala la ajira kwa vijana na kwa kweli katika wizara yetu ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo suala la vijana limebeba asilimia 70 ya utekelezaji wake katika ilani ya CCM, kwa sababu hata katika ibara ya 210(f) ya ilani ya CCM ya mwaka 2020 – 2025 imeweza kumzungumzia kijana atafaidika vipi na suala la ajira. Vile vile katika ilani yetu ya CCM imetoa ahadi kwamba itatengeneza takribani ajira laki tatu ili vijana wetu waweze kuajiriwa na inapozungumzia suala la ajira laki tatu inazungumzia ajira zilizorasmi na zisizorasmi lakini vile vile nazungumzia kumuwezesha kijana kuweza kujiari mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo niseme na niwaambie Waheshimiwa Wajumbe wizara yetu imejipanga vizuri kutengeneza miradi iliobora na sio miradi tu itakayotegemea bajeti kuu ya serikali bali ni miradi ambayo tutaibuni kuhakikisha kwamba tunatafuta wafadhili na wadau mbali mbali ambao watakuwa na uwezo mkubwa wa kuwasaidia vijana wetu waweze kujiajiri wenyewe lakini vile vile waweze kutengeneza ajira kwa vizazi vijavyo. Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo naomba nijielekeze kwenye suala zima la sanaa, burudani na michezo ambalo limeoneshwa katika ukurasa wa 34 wa hotuba hii ya Mhe. Rais. Mhe. Mwenyekiti, niseme tu katika hili ukienda moja kwa moja pia katika ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020 – 2025 ibara ya 187 na ibara ya 188

imezungumza kwa upana wake. Suala la kuendeleza sanaa, burudani na michezo pamoja na masuala ya kiutamaduni.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nataka tuelewe kwamba tunapozungumzia masuala haya tunazungumzia pia suala zima la mmomonyoko wa maadili. Hivyo niseme tu kwamba wizara yetu imejipanga vizuri kuhakikisha tunaendeleza vipaji, tunaendeleza sanaa yetu kama ni utambuzi au utambulisho wa nchi yetu lakini vile vile tutazingatia sana sauala la maadili ya Mzanzibari kwa kushirikiana na wizara nyengine ambazo ni wadau wa masuala haya. Vile vile ukienda katika suala la michezo ambalo ni pana sana lakini pia Mhe. Rais ametoa ahadi nyingi kwa wananchi wake wa Zanzibar kwamba atahakikisha anaimarisha suala la michezo lakini vile vile atahakikisha anasimamia timu na kuiboresha timu ya Taifa ya Zanzibar. Niseme wizara yetu ndio wizara husika moja kwa moja kuhakikisha inaimarisha timu hii ya Zanzibar.

Kwa hivyo tumejipanga vizuri kuwalea, kuwasimamia, kuwawezesha timu yetu ya Zanzibar iweze kufanya vizuri. Nataka niseme na nitoa ufafanuzi juu ya hoja ambayo aliijenga Mheshimiwa mwenzangu wakati akichangia alizungumza suala zima la masuala ya mpira na suala zima la *ZFF* na migogoro yake. Mimi nataka niwaambie kwamba wizara kama wizara tokea tulivyochaguliwa tumechukuwa hatua mbali mbali kuhakikisha tunakaa na *ZFF* na nataka niwaambie *ZFF* ipo katika ngazi mbali mbali. Ipo katika ngazi ya Taifa, Mikoa na Wilaya na mpaka sasa hivi tunachukua hizo jitihada za kuhakikisha tunaweka sawa kuanzia ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya, huku tukitambua kwamba zile sheria mama ambazo zimewekwa kwa ajili ya kusimamia mpira nchini kote moja kwa moja zinatoka na sheria za Kimataifa za *FIFA*, *CAF* pamoja na mashirikisho mengine yanayohusika na mpira wa miguu.

Wizara kama mlezi tunachukuwa hatua mbali mbali na niwaambie kwamba tunaendelea vizuri na nataka niwahakikishie haiwezi kufika miezi sita tutahakikisha *ZFF* imetulia inaongozwa kwa mujibu wa kanuni na utaratibu, lakini vile vile inaacha kuendesha mambo haya ya mpira kwa kutumia utashi zaidi, hilo tunalichukuwa na tunalifanyia kazi. Vile vile niseme kwenye suala zima la matumizi pia ya vyombo vya habari. Katika hotuba hii moja kwa moja haijaonyeshwa lakini ukienda katika ibara ya 123 na 124 ya ilani imezungumza juu ya suala zima la matumizi ya vyombo vya habari na mchango mkubwa katika kuleta maendeleo. Kwa hivyo kwa kumuunga mkono Mhe. Rais katika suala lake alilozungumza la matumizi ya teknolojia niseme wizara yetu tumejipanga vizuri.

Kwanza kuna mchangiaji mmoja pia alisema suala zima la kutumia masuala ya habari katika kutangaza utalii. Wizara yetu inashirikiana sana na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuhakikisha tuna-*promote* utalii wetu wa Zanzibar huku tukizingatia maadili na utamaduni wa mzanzibari. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme tu kwamba tutahakikisha tunamsadia Mhe. Rais lakini vile vile tutahakikisha hotuba yake hii tunaitekeleza na tutahakikisha tunasimamia kwa kile ambacho tumetakiwa kukisimamia kwa mujibu wa utaratibu na kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukuwe fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi lakini vile vile kuwashuku wajumbe kwa kuweza kunisikiliza na mimi natoa ahadi mbele yao kwamba niko tayari kushirikiano nao bega kwa bega katika kuhakikisha tunatekeleza ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025 kwani naamini ndio ambayo mahususi

imetuweka hapa kujadili mambo mbali mbali kuhakikisha ahadi zote tulizozitoa kama chama tawala tunazitimiza kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa na mimi naomba kuchukua fursa hii kushukuru sana familia yangu baba yangu mpendwa na mama yangu mpendwa pamoja na ndugu zangu wote wa karibu ambao wameweza kuniunga mkono katika milima na mabonde niliokuwa napitia katika safari yangu ya kisiasa hadi leo kuwa hapa katika jengo hili na kuweza kutoa mchango wangu kwa serikali yangu Mhe. Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nashukuru na naomba kuwasilisha. Ahsante.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe mchangiaji anaefuata ni Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, nimemtaja hapa pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ lakini simuoni kwa hiyo nitamuita Waziri wa Nchi Kazi, Uchumi na Uwekezaji atafuatiwa na Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *(S.W)* kwa kutujaalia asubuhi ya leo kuapata wasaa huu kwa kuja kuendelea kuchangia hotuba ya Mhe. Rais wetu mpendwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Pia nichukue nafasi hii maalumu kutoa pongezi maalumu kwa Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika, na wenyeviti wote kwa jinsi wanavyoendesha shughuli mbali mbali za Baraza letu. Naomba nichukuwe nafasi hii kwa dhati kabisa kumshukuru Mhe. Dkt Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake mbali mbali alizochukuwa za kuhakikisha kwamba Zanzibar yenye neema inafika na inakuja kwa haraka sana kwa sababu juhudi zake tunaziona ziko bayana. Nimpongeze kwa kuwateuwa Makamu wa Kwanza wa Rais Maalim seif Sharif Hamad na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdulla kwa kweli hakukosea kuwateuwa wasaidizi hawa wawili niwapongeze mawaziri wenzangu wote walioteuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hili ni Baraza langu la tano la uwakilishi nimeanza 2000 hadi leo *alhamdullillahi* nipo nashkuru Mungu. Sasa nimeshuhudia michango ya kila aina tokea Baraza la mwaka 2000 hadi leo 2021. Sitaki kusema yaliopita hayakuwa mazuri lakinin nasema jinsi ninavyoona Baraza hili mambo yanavyokwenda wengi wao ni vijana lakini inaelekea kuna khatima nzuri sana kwa vijana hawa huko tunakokwenda. Vijana nawapongeza sana kwa kweli wanachangia vizuri sana. *(Makofi)*

Nikishukuru sana Chama changu Cha Mapinduzi tokea mwaka 2000 kiliweka baraka zake kwangu mimi hadi uchaguzi wa mwaka 2020 kwa kunipitisha katika nafasi mbali mbali tokea nikiwa katika jimbo, Wilaya, Mkoa viongozi wote nawashukuru kwa kunipa imani hiyo na mimi nawaahidi sitowaangusha nitaendelea kukitumikia Chama changu Cha Mapinduzi na kuijenga nchi yangu kuhakikisha kwamba maendeleo ya haraka yanapatikana.

Lakini nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais aliyemaliza muda wake Dkt. Ali Mohammed Shein wa awamu ya saba ambae katika michakato yote ameshiriki kikamilifu, kabla ya hapo ni Dkt. Amani Abeid Karume ni Rais wa awamu ya sita ambae ndie alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi mwaka 2000 wakati ule ulipoanza mchakato wa kupitisha majina,

kwa hivyo namshukuru sana na yeye na nilifanya nae kazi kama ni Waziri wake kwa muda wa miaka kumi. Dkt Ali Mohammed Shein nimefanya kazi nae kwa miaka kumi na *inshaallah* Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi nina imani nae nitafanyakazi nae kwa kadri Mwenyezi Mungu atakaponijaalia *inshaallah*.

Kwa hivyo nawashukuru sana viongozi hao wote wamenipa mashirikiano makubwa sana nawashukuru sana Mawaziri wenzangu ambao tunaendelea kufanya kazi kwa pamoja. Nawashukuru Mawaziri ambao ni vijana mara nyingi huwa wananitafuta kuomba ushauri wa hapa na pale, nahakikisha kwamba niko tayari kuwasaidia kwa kila hali licha kwamba na wao wanafanyakazi vizuri. Lakini pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi wote kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya.

Mhe. Mwenyekiti, nina salamu maalum nimepewa na wananchi wa Jimbo la Makunduchi jana nilikuwa jimboni kwa sababu biashara asubuhi jioni unahesabu faida tu, ukisema hupiti jimboni kuna watu wanakwenda huko. Jana nilikuwepo jimboni nilikwenda kuzindua mradi wa maji katika kijiji cha Kibuteni na nimepewa salamu maalum nizipeleke kwa viongozi wetu, akiwemo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi na Makamu wake wote wawili, lakini pia kwa viongozi wote kwa jitihada zinazochukuliwa za kujenga Zanzibar yetu mpya. Kwa hivyo salamu hizi naomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, zimfikie Mhe. Rais na mimi mwenyewe nitamuandikia dokezo maalum kumshukuru kwa sababu ni salamu maalum nimepewa na wananchi nizipeleke na mimi sitaki kugombana na wananchi wangu kwa sababu bado mambo haya nayataka.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona jitihada hizo ulizochukua na sasa hivi tunaiona Zanzibar ilivyokuwa na umoja amani na utulivu tumshukuru sana kwa madhiriano haya yaliyofikiwa hivi karibuni, haya ni maridhiano namba mbili na kwa bahati nzuri mimi nishuhuda wa maridhiano ya mwanzo. Dkt. Amani Karume alifanya marekebisho ya Katiba ya mwaka 1984 na kuanzisha utaratibu wa kuwa na Serikali ya Umoja wa kitaifa kwa utaratibu uliowekwa kikatiba. Sasa Dkt. Ali Mohammed Shein alivyoingia madarakani mwaka 2010 akaanzisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Awamu ya Kwanza tukafika mpaka mwaka 2015 baadae mambo hayakwenda vizuri. Namshukuru sana Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi akaanzisha GNU awamu ya pili na hii inaelekea sura dhahiri kwamba tutakuwa na umoja na tutakuwa na nguvu za aina zote. Tumeona hapa waheshimiwa Wawakilishi wetu wa vyama mbali mbali hata vile vyengine kama mfano wa vyama vya ACT na vyenginevyo wakati wa kuchagua Mwenyeviti na viongozi wengine ndani ya Baraza wote walipiga kura za ndio kuunga mkono juhudi zile ambazo zimeamuliwa kwa pamoja, kwa hivyo hizi ni dalili njema na naomba tuendelee mitaani sasa hivi hali ni shuwari tunazungumza vizuri, tunafanya kazi kwa pamoja na tunajenga nchi yetu ni jambo la kupigiwa mfano sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri mimi nimeona GNU ya mwanzo na hii GNU ya pili nimeshuhudia vile vile *inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie safari hii idumu milele aendelee 2020 mpaka 2025 na Mungu amjaalie *inshaallah* kwa nia yake nzuri hii ikifika 2025 ataendelea mpaka 2030 tukijaaliwa *inshaallah.* GNU ina faida nyingi kwanza nchi kuimarika kwa umoja, mshikamano lakini pia kuleta utulivu katika nchi. Lakini tumeona katika hotuba yake Dkt. Hussein Ali Hassan alivyoelezea suala zima la utawala bora namna gani anapambana na wale wanaokula rushwa na wahujumu uchumi, wale wote waliokuwa hawawajibiki kazini na

watumishi waliokuwa wazembe. Hili tunampongeza sana na tunaliunga mkono asilimia mia moja na bahati nzuri masuala haya yote yako chini ya Wizara yetu Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na mimi naahidi kabisa haya nitayasimamia kwa nguvu zangu zote. Aidha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali nayo tutaimarisha kivitendo kuona kwamba nayo inatimiza wajibu wake ilivyo.

Tume ya Maadili ya Viongozi tunatoa shukurani maalum kwa Wajumbe wote kwa kukiri matakwa ya kikatiba na sheria vile vile ya kuweza kurejesha fomu zile kwa wakati Waheshimiwa wote tunakupongezeni sana kwa kazi hiyo, msiniulize kama kuna wengine hawakurejesha au wemerejesha lakimi mimi nasema wote wamerejesha hakuna mashaka yoyote.

Lakini pia nichukue nafasi hii kuahidi kivitengo kwamba sisi tutaitekeleza ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na ni wajibu wetu sote kufanya hivyo, hivi karibuni Mhe. Rais ameteua majaji wa Mahakama Kuu kwa ajili ya kurahisisha utaratibu wa kutoa kesi. Suala la Mahakama linamgusa sana kwa sababu anataka kesi ziende haraka sana zisicheleweshwe na hili suala la Mahakama vile vile liko upande wetu tunalisimamia sisi na hivi karibuni ameteua wale majaji wawili kwa kuongeza nguvu.

Mhe. Mwenyekiti, tayari nataka nitoe taaluma kidogo bado ni mwalimu na ualimu wangu haufutiki uheshimiwa siku moja utaondoka lakini ualimu hauondoki, tunakosea kidogo wakati mwengine tunaposema tumeanzisha Mahakama ya Udhalilishaji au tumeanzisha mahakama ya rushwa, hakuna mahakama ya udhalilishaji wala hakuna Mahakama ya rushwa isipokuwa kuna mahakama ya kupambana na udhalilishaji na Mahakama ya kupambana na rushwa na uhujumu wa uchumi. Tukisema kuna Mahakama ya Udhalilishaji maana yake kama hiyo Mahakama yenyewe ndio inadhalilisha, ukisema kuna Mahakama kuna mahakama ya rushwa inakuwa kama mahakama hiyo ndio inatoa rushwa, sasa hapa kidogo mimi naomba tuitengeneze mimi kwa ualimu wangu inaniambia tunakosea tukifanya hivyo, isipokuwa tunapambana na rushwa na tunapambana na udhalilishaji na nashukuru sana tayari Mahakama hizo Mhe. Rais kwa imani aliyokuwa nayo ya kuwahurumia watoto na wengine wote wanaodhalilishwa basi tayari Mahakama hii imeshaanzishwa. Hivi karibuni ametoa gizo vile vile kuwa na Mahakama ya kupambana rushwa nayo ianzishwe mara moja. Namuahidi kwamba mahakama hizo zitafanya kazi vizuri na Mahakimu hawa au majaji wako tayari kufanya kazi.

Lakini pia jambo la msingi ambalo limeimarika katika awamu hii ni suala zima la udhibiti wa fedha za umma, pesa sasa hivi watu wanaziheshimu na ni wajibu wetu kuziheshimu. Pesa sasa hivi inapatikana kwa shida hivyo inabidi tufanye kazi ya ziada. Tunakumbuka hapa mitihani tuliyoipata ya maradhi haya ya corona na matatizo mengine mengine, *inshaallah* Mwenyezi Mungu atuondoshee maradhi haya ili baadae tuendelee kufanya vizuri uchumi wetu kuimarika watalii wanakuja lakini vile vile tuendelee kuimarisha na maeneo mengine, uchumi wetu wa bluu uwe ni dira ya kutuongoza katika kuleta maendeleo ya nchi yetu na tujengeni nidhamu tushirikiane kwa pamoja.

Mwisho, nachukua nafasi hii kwanza nitakuwa sifanyi haki na mimi kwa sababu wenzangu wote wanashukuru familia zao na mimi nyumbani wanasikiliza nisije nikafika huko nikaambiwa wenzio wote wamepongeza watu wao wewe hujatupongeza, sasa ni vizuri na mimi sitaki

ugomvi, kuna msemo wa utani unaosema shikio lenyewe limeshafika mabegani yasije yakafika tumboni kwa kuvutwa kila siku.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukue nafasi ya kuwashukuru Alhamdullillahi familia yangu yote kwa kuniunga mkono katika mambo haya ya kisiasa, wawao familia sio watu wa siasa lakini mimi nilitumbukia katika siasa na alhamdullillahi nipo na naendele na ishaallah naahidi kuendelea mpaka pale Mwenyezi Mungu aliponiandikia, lakini vile vile niwashukuru wote niwashukuru wazee wangu baba na mama wameshafariki wametangulia mbele ya haki lakini walifanya *investment* kubwa ya kutuelimisha kutupeleka skuli kama si hivyo tusingefika hapa leo *alhamdullillah*. Ndugu zangu, watoto wangu bila ya kumsahau na juzi Mhe. Juma Ali Khatib alikuwa anasema kama timu ya Yanga imesherehekea miaka thamanini na tatu kwa sababu ilianzishwa tarehe 11 Februari, 1935. Ndio siku ambayo tulikuwa tunazungumzia mambo mengi sana lakini vile vile tarehe 11 Februari, 1981 na mimi ndio siku niliyofunga ndoa na juzi nimetimiza miaka 40 basi tuombeane Mungu tupate na 40 mingine inshaallah ili mambo yaende vizuri.

Baada ya kusema hayo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi Mhe. Mwenyekiti, naomba niipongeze hotuba hii kwa asilimia mia moja na tunaiunga mkono na kumtakia kila la kheri Rais wetu kwa kweli ana muelekeo mzuri sana na ni wajibu wetu sote kuunga mkono juhudi zake, *inshaallah* Mwenyezi Mungu atakusaidia. Nichukue nafasi hii kuwashukuru wote walionisikiliza nikushukuru na wewe Mwenyekiti kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Waziri sasa nimuite Mhe. Waziri wa Nchi, Kazi, Uchumi na Uwekezaji atafuatiwa na Waziri wa Kilimo Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na Mhe. Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi ajiandae.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika asubuhi hii ya leo kuweza kujumuika na Waheshimiwa Wawakilishi katika Baraza lako hili tukufu na kuweza kuchangia hoja ya Hotuba ya Mhe. Rais, hotuba ambayo imejaa hekima na busara na ambayo inatoa dira na mwelekeo wa nchi yetu wapi tulipo na tunapoelekea na hatimaye katika suala zima la kuboresha hali za wananchi wetu.

Lakini pili Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais kwa kazi kubwa na nzuri anayoendelea nayo kuifanya ya kutuletea maendeleo au kusukuma gurudumu la maendeleo katika nchi yetu, lakini vile vile nimpongeze ama niwapongeze viongozi ambao amewateua wakiwemo Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Hemed Suleiman Abdalla pamoja na kaka yangu Mwanasheria Mkuu wa Serikali yetu hii kijana mahiri na mchapa kazi Dkt. Mwinyi Talib.

Mhe. Spika, pia nijumuike na ndugu zangu Mhe. Abdulgulam na Mhe. Mihayo Nunga kwa kutoa shukurani zangu za dhati kwa mke wangu kipenzi Bi.Bahati Chibuye kwa kuendelea kuniunga mkono katika safari yangu hii na kuniunga mkono katika kutekeleza azma yangu ambayo ya kuwatumikia wananchi wa jimbo la Bububu, kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, mke wangu tumepitia mambo mengi sana licha ya muda mfupi wa ndoa lakini nimemuachisha kazi yake ambayo ilikuwa ni nzuri na inamlipa vizuri akiniunga mkono kuelekea visiwani Comoro wakati

nilipopangiwa kazi kule kama Afisa ubalozi, lakini baadae tukaondoka huko tukaingia katika masuala ya siasa ila bado ameamua kuendelea kuwa name, kwa hivyo namshukuru sana kwa uelewa wake na ustahamilivu wake. Lakini vile vile nimpongeze kwa kazi kubwa na nzuri anayoendelea kuifanya ya kuilea familia yetu changa kwa kweli watoto wetu wamepata mama bora.

Mhe. Mwenyekiti, pia kwa kipekee nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wangu wa jimbo la Bububu kwa kunichagua kwa kura nyingi sana na hatimae kuwa mwakilishi wa Jimbo la Bububu, nafahamu kwamba wengi wao sasa hivi inawezekana wanajiuliza kwamba Mhe. Mwakilishi kidogo amepotea, lakini niwahakikishie tu kwamba nipo nao bega kwa bega katika kutekeleza azma ya maendeleo ya jimbo letu, lakini nitaomba tu wanivumilie kutokana na kazi kubwa ambayo inatukabili huko Serikalini ila tutajitahidi kwa kadri ya uwezo wetu kupata ule uwiano na kuhakikisha tunatekeleza majukumu yetu kwa ufanisi na uledi mkubwa kwa pande zote mbili.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuchangia sasa hotuba ya Mhe. Rais na kama nilivyotangulia kusema hapo awali kwamba ni hotuba ambayo inatoa dira na muelekeo wa nchi yetu na namna ambavyo tunataka kusukuma masuala ya maendeleo na kuboresha hali za wananchi wetu. Katika suala la uwekezaji, suala la uekezaji ni suala mtambuka Wizara zote hizi inapokuja katika masuala yao ambayo yanayatekeleza kisekta mlango wao mkuu unaanzia katika suala la uwekezaji. Sasa kwa kutambua umuhimu huo kwa upande wetu sisi tumedhamiria kwanza kuboresha na kuweka ufanisi mkubwa sana katika Afisi zetu na Taasisi zetu kuhakikisha kwamba wawekezaji wetu wanahudumiwa kwa ufanisi mkubwa sana na masuala yao yanashughulikiwa katika muda mchache sansa ili kuwawezesha kupata vibali stahiki kwa ajili ya kuweza kutekeleza azma yao ya kuwekeza. Katika kufanya hivyo hatua ya mwanzo kabisa ambayo tumeanza kuichukua ni kuboresha kituo chetu cha huduma ya *one stop centre* ambacho kipo katika mamlaka ya uwekezaji *ZIPA.* Kituo hicho sasa hivi tunakijengea ufanisi na kwa hatua ambayo tumefikia mpaka sasa tumefikia asilimia 85% ya ufanisi bado kuna mambo mawili matatu ambayo kwa kushirikiana na ndugu yangu hapa Mhe. Waziri wa Fedha tutaweza kufikia asilimia mia moja mara baada ya kuweka ile mifumo yetu vizuri na kuhakikisha kwamba huduma zote zinapatikana katika eneo hilo.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyofahamu suala la uwekezaji linaenda sambamba kabisa na suala la upatikanaji wa ardhi na tunafahamu kwamba nchi yetu ni ya kisiwa, watu wetu wanaongezeka lakini nchi haiongezeki kwa ukubwa kwa hivyo kuna haja kubwa sana kuangalia namna gani ambavyo tunaweka vizuri maeneo yetu kwa kuyapangilia matumizi yake, ili hata wawekezaji wanapokuja basi wasiwe wanasumbuka katika kupata maeneo kwa ajili ya uwekezaji. Hivi sasa kuna changamoto kubwa wawekezaji wengi wanapokuja wanakuwa tunakuwa tunashindwa kuwabainishia maeneo kwa ajili ya uwekezaji licha kwamba maeneo hayo yapo lakini kwa sababu ya kukosa mipango maalum inakuwa vigumu. Kwa hivyo katika kutekeleza hilo sasa Serikali ya awamu ya nane imedhamiria kutengeneza kitu ambacho kinaitwa *Land Bank* jambo ambalo ameligusia Waziri wa Ardhi tunashirikiana kwa pamoja kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapata hiyo *Land Bank* ambayo sasa itakuwa chini ya Mamlaka ya *ZIPA* na itarahisisha upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji wetu na kupunguza ule muda wa kutoa *lease* kwa wawekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, jambo kubwa ambalo linachelewesha wawekezaji kupata vile vibali stahiki ni suala la kupata *lease* ya ardhi, anawezekana akapata kibali chake *certificate* ya uwekezaji ya *ZIPA* ndani ya kipindi cha wiki moja mpaka mbili lakini ucheleweshaji mkubwa unaotokana na kupata *lease* ya ardhi ambayo sasa hiyo inaweza kuchukua hata miaka miwili mpaka miaka mitatu. Sasa kwa kasi ambayo tunataka kwenda nayo hatuna budi kurekebisha kadhia hiyo ili kuhakikisha kwamba jambo hilo linaratibiwa kwa ufanisi mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile katika suala la kujipanga juu aina ya uwezekezaji ambao tunauhitaji, tunahitaji kuweka *gidelines* maalum kwa ajili ya wawekezaji wetu, tunapokea maombi mengi sana ya wawekezaji ambao wanakuja binafsi mpaka sasa hivi nafikiri nimeshapokea wawekezaji hawapungui 60. Lakini kama nchi lazima tuwe tuna muelekeo wa aina ya uwekezaji ambao tunawataka ili kurahisisha, lakini vile vile kutoa taarifa za awali kwa wale wawekezaji kabla hawajaja watambue kwamba kuna fursa gani ambazo tunazo sisi kama nchi na vipaumbele vyetu viko katika maeneo gani, kwa mfumo huu ambao tunakwenda nao tunakuwa hatuna mwelekeo maalum, matokeo yake unajikuta unapokea wawekezaji ambao saa nyengine ni madalali tu au wawekezaji hewa. Kwa hivyo kitakwimu utaonekana kwamba watu waliokuja walioliza ni wengi lakini utekelezaji unakuwa ni mdogo. Sasa tulipokuwa tumetoa hii *investment gideline* itakuwa imeturahisishia kazi yetu kwa maana hiyo mtu kabla hajaja tayari atakuwa ameshapitia *guarline* yetu na anajua kwamba ukienda Zanzibar maeneo ya uwekezaji ni haya, vipaumbele vya Serikali ni hivi na yeye atakuwa anajijua jinsi gani vya kujipanga.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, niliarifu tu Baraza lako tukufu kwamba tupo katika hatua ya kuandaa *gideline* hiyo ambayo itamrahisishia hata Mhe. Rais pindipo atakapokuwa anafanya ziara zake nje ya nchi kwamba hana haja tena sasa ya kumtafuta Mhe. Waziri wa Sekta husika au Katibu Mkuu wa sekta husika, matokeo yake atakuwa na ile *gideline* ambayo anaweza akaiacha pale ambayo itakuwa ni muongozo wa kutosha kabisa kwa ambae anataka kuja kuwekeza.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri una dakika mbili.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, basi kwa kumalizia tu labda niseme katika suala la kazi kwa maana ya Kamisheni ya Kazi, tunajaribu kuendelea kuwajengea uwezo maafisa wetu kazi, kuhakikisha kwamba na wao wanatekeleza kazi zao kwa ueledi na kwa ufanisi mkubwa, tunafahamu kuna changamoto nyingi za ajira katika maeneo yetu mbali mbali, kwa ajili ya wale ambao hawatoi mikataba ambayo inaeleweka au wanafukuza wafanyakazi bila ya kuzingatia taratibu au sheria za kazi zilizopo nchini. Kwa hivyo ni jukumu letu sisi tumeliona kwamba tuongezee ujuzi maafisa kazi wetu lakini vile vile kuwasisitizia kwamba waepukane na suala la rushwa. Maana hili ni jambo ambalo limekuwa likilalamikiwa sana na waajiri kwamba maafisa kazi kidogo vibahasha vimekuwa ni vingi sana, lakini tumeshaelekezana katika jambo hilo kwamba hatutovumiliana hata kidogo linapokuja suala zima la kulinda nidhamu kwa afisa kazi kuhakikisha kwamba anatekeleza wajibu wake kama inavyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mfuko wa uwezeshaji tunaendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya mfuko huo lakini vile vile kuweka mikakati ya kutanua wigo wa mfuko huo ili kuweza kuwafikia watu wengi zaidi ili waweze kukopa, kwa sasa hivi tunafahamu kwamba mahitaji ni makubwa kuliko uwezo wa mfuko, lakini naamini kwamba tutakapomaliza

kukamilisha taratibu zetu pamoja na kuunda ile kamati ambayo itasimiamia suala la utanuzi wa ule mfuko basi tutauongezea uwezo wa kutosha ili kuweza kuwafikia wananchi wengi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia naomba na mimi nichukuwe fursa hii tena kuunga mkono hoja ya Mhe. Rais na hotuba yake nzuri na kuendelea kusisitiza tu kwa wajumbe pamoja na mawaziri wenzangu kwamba tuendelee kushikiriana hasa kwa upande wa Wizara ya Kazi, Uchumi na Uwekezaji, kwa sababu kama nilivyotangulia kusema ni wizara ambayo mtambuka inayogusa wizara zote kwa hiyo, tunahitaji kufanya kazi kwa karibu sana kwa mashirikiano makubwa ili kuweza kufikia azma na malengo yetu ya kuleta maendeleo ya kweli katika visiwa vyetu. Ahsante sana mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Waziri sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo atafuatiwa na Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ajiandae.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuniruhusu kuchangia Hotuba ya Mhe. Rais Hussein Ali Hassan Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika uzinduzi wake wa Baraza la Kumi la Wawakilishi la tarehe 11 Novomba, 2020.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimpongeze Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kuchaguliwa kwa asilimia 76.2 kwa nafasi ya urais wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nikipongeza chama changu kwa kumteua Spika, pamoja na Naibu Spika, katika Baraza lako hili tukufu, pia nimpe shukrani nyingi Rais kwa kumteua Mhe. Hemed Suleiman kuwa Makamu wa Pili na Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile nimshukuru Maalim Seif Sharif Hamad kwa kukubali kuunda Umoja wa Kitaifa kuwa na amani katika kisiwa chetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumchagua Dkt. Mwinyi Talib Haji kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye hili ni jembe la kuotea mbali. *(Vicheko)*

Mhe. Mwenyekiti, nakipongeza chama changu Chama Cha Mapinduzi kwa kuwachagua mawaziri walio mahiri katika ufanyaji wa kazi zao za serikali, lakini vile vile nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapiduzi kunichagua kuwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyohamu kilimo ndio uti wa mgogo wa taifa hili karibu asilimia 40 ya wananchi wameajiriwa na sekta hii na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanategemea sekta ya kilimo katika kujikimu kimaisha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitajikita zaidi kuhusu mambo yangu ya kilimo serikali itaendeleza mikakati iliyoandaliwa na serikali ya awamu ya saba yenye lengo ya kuongeza uzalishaji wa mawazo na kijitosheleza kwa mahitaji ya chakula, katika mikakati yetu ni kuendeleza mpango mkuu wa umwagiliaji maji Zanzibar ambao ni *Zanzibar Irrigation Master Plan* wenye kuhamasisha kuwepo kwa hekta 8,521 zinazofaa kujengewa miundombinu ya maji. Lakini katika mikakati mengine ni kuendeleza na kuimarisha huduma ya za ugani kwa kuwaajiri wataalamu wa kutosha na kutoa vifaa viinavyohitajika katika ukulima.

Mikakati mengine ni kuendeleza, kuhimiza kilimo cha kisasa cha uzalishaji wa mazao kwa kuwawezesha vijana kuendeleza na kilimo cha ujenzi wa vitalu nyumba ambao ni *green house*, pia ni kuweka mkazo katika kuwapatia wakulima pembejeo za kilimo, dawa za kuulia gugu na kuwapatia huduma bora za matrekta kwa ajili ya uchimbaji na uburugaji wa mashamba yao.

Taasisi ya utafiti ya kilimo kuhamasisha kukiendeleza kilimo cha Zanzibar na kusaidia upatikanaji wa masoko na mazao yanatokana katika kilimo hicho, lakini vile vile kuendelea na kuimarisha zao la karafuu kwa kuwapa mikopo wakulima na kutafuta masoko zaidi ya zao hili duniani.

Mhe. Mwenyekiti, mikakati mengine kusimamia na kuendeleza programu za kufufua zao la minazi la kuotesha miche ya minazi kwa visiwa vyote vya Unguja na Pemba, kama milivyosikia kwamba tayari tumeshatoa tangazo la kusimamisha madafu yote ya minazi mirefu na kuruhusu minazi mifupi au minazi ya kitamli katika kutekeleza agizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, katika ufugaji kutakuwepo mkazo katika kuendeleza shughuli za ufugaji wa kisasa ili kuongeza tija na mchango wa sekta hii katika upatikanaji wa lishe bora na kuimarisha pato la taifa, lakini vile vile ni kuhakikisha kuwepo matumizi mazuri za pembejeo za mifugo, dawa za chanjo na utoaji wa elimu juu ya matumizi ya mbegu bora za mifugo ambao tunatumia kwa ajili ya upandishaji wa ngómbe kwa shindano. Lakini vile vile tuna mikakati ya kubuni na kutekeleza mikakati na kukabiliana na vitendo vya wizi wa mifugo kwa kutumia sheria ambayo inafaa.

Mhe. Mwenyekiti, tuna mpango vile vile kuendeleza sekta ya mifugo kwa kuwakaribisha wawekezaji wakubwa waufugaji hasa wa ngómbe na mbuzi wa maziwa ambao wataweza kuwasaidia wafugaji wadogo katika kuzalisha bidhaa nyengine zinazotokana na mifugo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia pia niwashukuru familia yangu kwa ustahamilivu mkubwa katika kipindi chote cha wakati wa uchaguzi, lakini vile vile niwashukuru viongozi wangu wa Chama Cha Mapinduzi kwa Tanzania nzima. Niwashukuru wananchi wa Jimbo la Paje kwa uvumilivu wao wakati wa kampeni zote za Chama Cha Mapinduzi kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo la Paje tunaikubali hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia ahsante mwenyekiti. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Waziri sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi atafuatiwa na Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini na baadaye nitampa nafasi Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha sote sisi hapa kufika leo hii hapa.

Pili Mheshimiwa naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii lakini pia naomba pekee niwashikuru wananchi wa Jimbo la Mkoani kwa kuniteuwa au kunichagua kwa kura nyingi katika uchaguzi uliopita.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikishukuru chama changu cha CCM kwa kuniteuwa pia kuwa mgombea wa chama hicho katika uchaguzi uliopita. Mwisho na kwa kipekee naomba nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuniamini na kuniteua kuwa waziri wa wizara hii ngumu na nzito.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba nijielekeze katika mchango wangu kwa kutafsiri kwa vitendo hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar, katika tafsiri hiyo mheshimiwa naomba nijielekeze zaidi katika kuweka mambo matatu bayana.

Mheshimiwa Wizara yangu tumejikita kwanza katika kutekeleza suala hili ni kwanza tumejihisi kwamba ni lazima turekebishe au tuziboreshe sheria na taratibu za Zanzibar kwenye masuala ya bahari. Katika kufanya hili mheshimiwa tunataka tuangalie kwanza masuala ya bahari ni masuala ya kimataifa ambayo ni lazima tuangalie kwamba masuala ya bahari yanaendana na mikataba ya kimataifa *International Conversion and Protocol,* sasa sheria zetu ni lazima tuziboreshe ziendane na mikataba yote ambayo Tanzania imeingia kama imeweka sahihi hilo la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili ni suala la *Maritime System and Security* ulinzi na usalama wa bahari. Hitu hili mheshimiwa ni suala zito na linahitaji kuwekewa mikakati karibu sana bila ya kuhakikisha kwamba bahari yetu ni salama suala la uchumi wa bluu halitoweza kufanyika kama tulivyokusudia.

Mhe. Mwenyekiti, la tatu suala la mazingira. Mazingira yetu ya bahari ni lazima tuyahifadhi kuhakikisha kwamba tunakwenda katika maeneo ambayo lengo letu linafanikiwa ni lazima tuhakikishe kwamba mazingira ya bahari yanalindwa ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imejikita zaidi katika maeneo hayo katika masuala ya kuhakikisha kwamba tunafikia lile lengo alilokusudia Mhe. Rais. Sasa mheshimiwa, wajumbe wengi wameizungumza wizara yangu na kwa vile wizara yangu ndiyo wizara mama katika masuala maendeleo ya awamu nane, sasa nataka nieleze tu maeneo ambayo wajumbe wengi wamejaribu kuyazungumza.

Eneo la kwanza ni suala la wataalamu wa uchumi wa buluu wapatiwe elimu ya vitendo. Mheshimiwa hili ni suala ambalo ni la lazima katika elimu ya baharini ni lazima kwanza wataalamu wote wapate elimu ya vitendo, sasa hili tutalihakikisha tunakwenda kuungana na taratibu na sheria zilizowekwa.

La pili, elimu kwa wananchi kwa uchumi wa buluu, limesisitizwa na karibu wajumbe wote elimu ya uchumi wa buluu bado haijaeleweka nikiri kweli hili suala ni jipya lakini tunaenda nalo na tunaenda kidogo kidogo.

Suala la Tatu mheshimiwa suala la *Private Sector Participation* namna gani tunawashajihisha wawekezaji binafsi. Mheshimiwa nataka nikueleze sera yetu ya serikali ya awamu ya nane kwamba uchumi wa buluu uendeshwe na *Private Sector* na ushahidi nafikiri tumeuona karibuni tu tumesaini mikataba ya kimataifa na watu wa *Private Sector* wanataka kujenga bandari ambazo ni mfano kwa Afrika, bandari ambayo itagharimu karibu Dola bilioni sita, hizi zote zinagharimiwa na *Private Sector*.

Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wengi walitaka taasisi za uchumi wa bluu zijengewe uwezo tulikubaliana nao na tumeanza kufanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo. Viwanda vya uchumi wa buluu vizalishe bidhaa ziendazo na soko. Ni kweli mheshimiwa tunaelekeza kuweka viwanda vya kushindika samaki ambao tayari tunalo soko la ndani la kimatifa.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu nyengine wavuvi wanakwenda baharini kama wezi. Hili mheshimiwa limeelezwa na Mhe. Hamad kwamba baadhi ya wavuvi wanakuwa *harass*. Sasa hili nataka nilieleze kwamba, hakuna *harassment* katika wizara yangu wala hakuna *harassment* ya mvuvi yoyote, kinachofanyika ni kwamba baadhi ya wavuvi hawataki kufuata taratibu na ni lazima tuhakikishe kwamba nchi hii inakwenda kulingana na taratibu na sheria tulizojiwekea. Diaspora Wazanzibari walioko nje nafasi hii Mhe. Rais ameshaitangaza.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Diaspora Mhe. Rais amelitangaza hadharani kwamba anawakaribisha wananchi wote wa Zanzibar waliopo nje kushirikiana na serikali yao ili kuweza kuja kushirikiana katika suala la uchumi wa buluu.

Mhe. Mwenyekiti, ulinzi wa bahari katika maeno ya hifadhi hili tumelifanyia kazi tayari tumeshatoa boti za doria ambazo kuwa tayari sasa hivi zinafanya kazi katika maeneo ya hifadhi ya Minai, Mnemba na nyengineo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri una dakika mbili za kuhitimisha.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante baadhi ya wajumbe walitaka usafiri wa bahari ni lazima uimarishwe hili ni suala ambalo mheshimiwa tunalifanyia kazi kama nilivyosema usafiri wa bahari, usafiri wa kimataifa utafuata taratibu wa kuhakikisha kwamba masuala ya usalama yanaimarishwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba nitamke naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nakushukuru mheshimiwa. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri ahsante mchangiaji anayefuata ni nilimtamka Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini lakini naomba sasa nimpe nafasi Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ atafuatiwa na Waziri wa Maji na Nishati na baadaye Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ajiandae.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa ruhusa yako naomba sasa nichangie hoja ilikuwa mezani kwetu ya hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa wakati akizundua Baraza la Kumi la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya na uzima tukawepo hapa, lakini pia nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa ushindi mkubwa alioupata wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Shughuli za Serikali na Mhe. Makamu wa Kwanza kwa dhamana hizo kubwa katika nchi yetu, sambamba na hilo nichukuwe fursa hii pia kukipongeza kwa dhati changu Chama Cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa ulioupata katika uchanguzi mkuu.

Kipekee niwashukuru wananchi wa jimbo langu wananchi wa Jimbo la Ole kwa maamuzi yao ya busara ya kuamua kunichagua kuwa mwakilishi wao na kunipa dhamana katika chombo hiki muhimu, lakini pia niwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi wote na wao kwa nafasi zao kwa kuchaguliwa katika majimbo yao pia niwapongeze wote waliopewa dhamana za kiutendaji katika awamu hii ya serikali ya nane, wakiwemo Waheshimiwa Mawaziri wote, wakiwemo na watendaji wengine.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi kabla ya kuanza kuchangia kwanza niseme kwamba naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, kimsingi hotuba hii itaendelea kubakia miongoni mwa hotuba muhimu yenye lengo kubwa ya kuitoa nchi yetu ilipo na kuipeleka mbele zaidi. Hotuba hii ni yetu sote, hotuba hii inawagusa mawaziri, hotuba hii inawagusa Waheshimiwa Wawakilishi, hotuba hii inawagusa watendaji, hotuba hii inamgusa mkulima, mkwezi, mfanyakazi na kila mwananchi anayeitakia mema nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba hii imegusa sekta ya kiuchumi, zimegusa sekta ya kijamii na kisiasa. Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi huo tuseme ukweli hotuba hii itabakia kuwa ni alama isiyofutika katika nyoyo za Wazanzibari wote. Hakuna mpenda amani, mpenda maendeleo ya nchi hii anaweza kuisahau hotuba hii, na kama kweli tumeamua kutaka kuitendea haki hotuba hii basi tuibakize hotuba hii kuwa hadudi rejea ya mipango yetu yote ya kimaendeleo. Hatuna eneo la kisekta iwe la kiuchumi au kama ni suala la kisiasa tunaweza tusiitumie hotuba hii kwa ajili ya kuleta mustakabal mwema kwa ajili ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, yameguswa masuala ya kodi, yamegushwa masuala ya utalii, viwanda, kilimo na sekta nyengine zote tusipoenda kuitekeleza hotuba hii katika maeneo yaliyoainishwa, basi maeneo yote hayo utekelezaji wake utabakia kuwa ndoto. Ukisoma ukurasa wa 30 kwenye hotuba hii Mhe. Rais ameonesha dhamira yake ya dhati kutaka kujenga misingi ya utawala bora kwa kupambana na vitendo vya rushwa. Vita hii si vita ya wizara moja, vita hii si vita ya wawakilishi, vita hii si ya Mhe. Rais peke yake. Kwa hivyo, kama kweli tumedhamiria kuitendea haki hotuba hii ni vyema tukashirikiana katika kuviendeleza vita hivyo katika sekta zote. Itabakia kuwa ndoto tukizungumzia ukusanyaji wa kodi halafu kodi hiyo ikawa kuna watu ama kuna wala rushwa wanaidokoa kodi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika wizara ninayoisimamia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ katika kuitendea haki hotuba hii ya Mhe. Rais tumejipanga kuboresha kama ilivyoanishwa katika hotuba hii mazingira mazuri ama mabadiliko muhimu ndani ya Idara Maalum za SMZ. Mhe. Mwenyekiti, katika kuleta mabadiliko hayo moja tutaendeleza kujenga misingi ya kinidhamu, lakini mbili kuendelea kuwalea kwa kuwapatia mafunzo wanayostahiki watendaji au wapiganaji waliomo katika idara zetu zote tano maalum.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika wapiganaji hawa wamekuwa wakifanya kazi kubwa wakati wote nchi yetu imebakia kuwa shwari kwa mchango mkubwa wanaoutoa katika kulinda nchi yetu hii. Tunawajibu wa kuboresha mazingira yao katika utendaji wao wa kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, pia tutahakikisha kama wizara ambayo inasimamia ama wizara ambayo ni Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kuondoa lile ambalo Mhe. Rais amelizungumza kwenye hotuba hii, suala la urasimu. Mhe. Mwenyekiti, tumejipanga kuhakikisha kwamba huduma zinazotolewa ndani ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali na Idara Maalum za SMZ katika kuunga mkono hotuba hii ya Mhe. Rais tunaondoa urasimu wa upatikanaji wa huduma hizo.

Mhe. Mwenyekiti, tumeanza kufanya hivyo maeneo yote ambayo tumekasimiwa madaraka ya kutoa huduma kwa ajili ya wananchi wetu tutajenga misingi ya utoaji huduma hizo, moja ziwe bora lakini mbili zisiambatane na viashiria vya aina yoyote vya urasimu.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba hii ya Mhe. Rais imegusia suala la utawala bora, suala la utawala bora ni suala mtambuka ukienda kilimo lipo, ukija Tawala za Mikoa lipo na ukienda uwekezaji lipo. Kwa hiyo, katika kuitendea haki hotuba hii na kumuunga mkono Mhe. Rais tutahakikisha ndani ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum tunajenga misingi ya utawala bora kwa kukemea na kwa kuviondoa vitendo vyote vyenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu wa mali ya umma, kutokuwajibika, uzembe na yote ambayo yanakinza misingi ya utawala bora. Tukifanya hivyo tunaamini kwamba tutakuwa tumeitendea haki hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, katika kujenga mazingira mazuri kwa wananchi wetu, Mhe. Rais katika hotuba yake hii alizigusia barabara za ndani tumeanza kuchukua jitihada. Tumeanza kuchukua jitihada za kuzifanyia upembuzi yakinifu barabara hizo kwa kuzitambua ili jitihada za makusudi sasa zichukuliwe katika kuzitengeneza barabara hizi. Tunaamini kwamba tukishakujua tatizo lilipo ni rahisi kuzitatua. Kwa hiyo, kwa vile hotuba hii tumesema ni miongoni mwa hadidu rejea ya uendeshaji wa wizara yetu, tutahakikisha kwamba tunatekeleza jukumu hilo la kuzifanyia matengenezo barabara hizo za ndani zilizoainishwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hotuba hii imeshachangiwa na walio wengi niendelee kusema kwamba tunaunga mkono hoja hotuba hii, lakini pia tuendelee kukupongeza na wewe kwa kukalia kiti hicho kwa mara ya kwanza na kuonesha ule ujasiri wa mamlaka uliopewa na kuyatumia vile inavyotakiwa. Tukutakie kila la kheri na tuhakikishie na sisi tutakupa mashirikiano yetu ya dhati, nimalizie kwa kumshukuru tena Mhe. Rais kwa dhamana hii kubwa aliyonipa kwa ajili ya kutumikia taifa letu. Niwahakikishie wananchi na nimuhakikishie na yeye tutafanya kazi mpaka tone letu la mwisho la damu kwa maslahi ya nchi hii.

Baada ya kusema hayo niunge mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Waziri na mimi nimepokea pongezi nakushukuru sana, Waheshimiwa Wajumbe sasa namwita Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini atafuatiwa na Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na baadae nitampa nafasi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwa kadri hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa katika Baraza hili siku ya tarehe 11 Novemba, 2020.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kutujaalia kuwa wazima leo hii kuendelea na shughuli zetu za ujenzi wa taifa hili. Tukikumbuka kwamba tukiwemo humu wenzetu wengi wamepoteza maisha tuwaombee kwa Mwenyezi Mungu alaze roho zao mahala pema peponi, na sisi ambao tupo atupe mwisho mwema.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake imara, makini na shupavu ambapo ndani ya siku mia za uongozi wake tumeanza kushuhudia mabadiliko makubwa ya kimaendeleo na muonekano wa maendeleo makubwa zaidi yajayo katika siku za mbele. Aidha, nimshukuru kwa kuamua kwa makusudi kutimiza wajibu wake wa kikatiba kwa kuunda serikali ya pamoja, serikali ambayo imeondoa kwa kiasi kikubwa manung'uniko lakini na chuki ambazo zilikuwepo baina ya watu. Naomba nimpongeze sana Mhe. Rais kwa hili alilolifanya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze kwa uteuzi alioufanya kwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais hiki ni kielelezo tosha cha ukomavu wake katika uongozi, pia katika kujenga demokrasia na umoja wa nchi yetu. Nimpongeze kwa uteuzi wa mawaziri aliowateuwa, mawazi ambao nao wameanza mchaka mchaka kumsaidia Mhe. Rais utekelezaji wa hotuba yake aliyoitoa, ahadi zake pamoja na ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, kipekee naomba pia nitoe shukurani na pongezi kwa wananchi wa Jimbo la Chonga Wilaya ya Chake Chake, Mkoa wa Kusini Pemba kwa kuonesha imani yao kwangu, imani yao kwangu pia ni imani kwa Rais wa Zanzibar na ni imani kwa Wazanzibari. Naomba niwahakikishie kwamba nitawatumikia kwa nguvu zangu zote kuhakikisha kwamba naleta mabadiliko ndani ya Jimbo la Chonga na ndani ya Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba imesifiwa sana ni hotuba nzuri na mimi nilikuwa nikijaribu kupitia baadhi ya hotuba nyingi ambazo zimewahi kutolewa zikiwa nzuri lakini naweza kusema kwamba hii ni hotuba ya karne. Ni hotuba ambayo imejaa busara, hekima lakini na ujasiri kwa yale ambayo ambayo yamelezwa katika hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako sasa naomba nielekee kwenye maeneo mbali mbali na nitagusia maeneo machache kwa sababu maeneo mengi yamegusiwa. Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze na eneo la maji.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye hotuba yake Mhe. Rais ameeleza upatikanaji wa huduma hii lakini pia na changamoto zilizopo, naomba na mimi niseme kwamba changamoto hizo zipo lakini tunaendelea kuzipatia ufumbuzi siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Maji, Nishati na Madini imejipanga kuhakikisha kwamba inaondoa changamoto hizi za huduma hii muhimu ya maji safi na salama kwa kujenga miundombinu iliyo imara zaidi ikiwemo ujenzi wa matangi ya kuhifadhia maji pamoja na kulaza mabomba katika sehemu mbali mbali za visiwa hivi vya Unguja na Pemba pamoja na visiwa vyake vidogo vidogo kuhakikisha kwamba hali ya upatikanaji wa huduma hii inakuwa nzuri na bora zaidi.

Aidha, tumejipanga kuendelea kutatua changamoto zote za upotevu wa maji ambayo imeonekana kwamba miundombinu chakavu ni chanzo kikubwa cha upatovu wa maji na kupelekea upungufu mkubwa wa upatikanaji wa huduma hii kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, tunao mpango wa kuhakikisha kwamba tunafunga mita katika maeneo mbali mbali ya mitaa ili kupata tathmini hasa ya uzalishaji wa maji tunaozalisha lakini pia yale maji yanayopotea ili kujiweka vizuri zaidi kuhakikisha kwamba huduma hii inawafikia wananchi na kuondoa yale malalamiko ambayo yamekuwa yakijitokeza kwa muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi naomba nijielekeze kwenye huduma ya nishati ya umeme. Mhe. Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa huduma hii inapatikana katika maeneo mengi ya Unguja na Pemba, lakini zipo changamoto ndogo ndogo ambazo zimekuwa zikijitokeza siku hadi siku na wizara yangu kupitia Shirika la Umeme itahakikisha kwamba inafuatilia kwa karibu hitilafu hizi na kuzifanyia marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia hotuba ya Mhe. Rais pamoja na ilani ya Chama cha Mapinduzi ni kutafuta umeme wa uhakika au nishati mbadala ya umeme. Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa hotuba hii ambayo imetolewa mwezi Novemba na Mhe. Rais tumeanza utekelezaji wake kwa kuingia mikataba ya awali pamoja na kampuni ambayo imeanza upembuzi yakinifu kwenye uzalishaji wa umeme na gesi asilia.

Mhe. Mwenyekiti, uwepo wa umeme wa uhakikika ni moja kati ya *incentive* za uwekezaji hapa kwetu. Kwa hiyo, kupitia Wizara ya Maji na Nishati tumejipanga kuhakikisha kwamba tunakuwa na umeme wa uhakika na wa kutosha hapa visiwani ili iwe ni kivutio kikubwa cha uwekezaji katika nchi yetu. Pia itapelekea kuongezeka kwa ajira, zile ajira ambazo tulizinadi katika ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ajira 300,000 zitatoka miongoni mwa maeneo haya ya uwekezaji ambayo yanaanza utekelezaji wake muda...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri dakika mbili malizia.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema kwamba na mimi nichukue fursa hii kumuhakikishia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwamba tutasimamia utawala bora katika Wizara ya Maji na Nishati pamoja na wizara nyengine kuhakikisha kwamba wale wote wabadhirifu, wala rushwa na wizi tutawashughulikia kwa mujibu wa taratibu za kisheria. Aidha, kwa kipekee Mhe. Mwenyekiti

naomba niseme tu kwamba tunamuhakikishia Mhe. Rais kwamba tutajitahidi kadri ya uwezo wetu kuhakikisha kwamba amani ya nchi hii inaendelea kusimama, inadumishwa kwa maslahi ya Wazanzibari wote.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naomba Mwenyezi Mungu atuongoze katika kufikia haki na amuongeze Mhe. Rais aweze kutuongoza na kusimamia yote ambayo ameyaeleza katika hotuba yake, ameyaeleza katika ahadi zake pamoja na ilani ya Chama cha Mapinduzi eeh Mwenyezi Mungu ibariki Zanzibar, Mungu ibariki Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Waziri sasa naomba nimwite Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi ningependa kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, mwenye kurehemu kwa neema ya uhai na uzima na tukakutana leo hii hapa katika mwendelezo wa vikao vya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, pili ningependa kuchukua nafasi hii kwa dhati kabisa kumshukuru Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuniteuwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, kwa hakika kwangu ni heshima kubwa na nitaienzi katika kuhakikisha kwamba nafanya kazi zangu kwa mujibu wa sheria, katiba na taratibu ambazo zimewekwa.

Pia nipende kuchukua nafasi hii kumpongeza yeye Mhe. Rais kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa hakika ni imani kubwa sana ya wananchi na ni imani ya wananchi kwamba tutapata mafanikio ambayo tunatarajia kama kauli mbiu inavyosema “Yajayo Yanafurahisha”.

Pia ningependa kuchukua nafasi hii kuwapongeza makamu wetu wawili, Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad na Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Hemed Suleiman Abdalla kwa kuteuliwa kuwa wasaidizi wakuu wa Mhe. Rais. Kwa hakika ni imani kubwa sana ambayo Mhe. Rais anayo kwao wao na kwa hakika kwa uwezo ambao wanao watakuwa wasaidizi wakubwa sana wa Mhe. Rais.

Vile vile nitoe pongezi kwa mawaziri na viongozi mbali mbali walioteuliwa na Mhe. Rais katika kumsaidia kazi na kuona kwamba wanakuwa sehemu ya historia. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote walioteuliwa katika kukiongoza chombo hiki kikuu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka nijielekeze katika kutoa michango yangu na hasa baada ya shukurani hizo kumpongeza kwa dhati pia Mhe. Rais kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa siku ya Jumatano, tarehe 11 Novemba, 2020 katika Uzinduzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi hoja ambayo ilitolewa na Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum. Katika hotuba hiyo kwa hakika Mhe. Rais ametuonesha dira ya wapi tulipo na wapi tunapotaka kuelekea, imeitwa majina mengi sana

hotuba hiyo ikiwemo *Golden Speech* na kwa hakika imesadifu kweli kuitwa kuwa ni *Golden Speech*. Lakini pia unaweza ukaita kwamba ni *Speech of the Millennium* kwa sababu inatoa dira na imekuwa kama *cyclopaedia* ya kuonesha kila sehemu, kila Nyanja nini ambacho kinatakiwa tukifanye kwa maslahi mapana na maendeleo ya nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wangu mimi nitajielekeza zaidi katika kuangalia taratibu za mikataba pamoja na sheria mbali mbali ambazo Wajumbe wako wa Baraza hili tukufu wamejadili na mawaziri wenzangu baadhi wakatilia umuhimu huo ambapo na mimi nataka kutilia msisitizo katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba ya Mhe. Rais katika kitabu chake cha hotuba tunapochukua ukurasa wa 10 mpaka 16 unaoanza kuzungumzia Uchumi wa Buluu au Uchumi wa Bahari na namna ambavyo umefungamana na sekta za uvuvi, utalii, mafuta na gesi pamoja na bandari. Ni wazi kwamba Mheshimiwa upo umuhimu wa kuzingatia upya kwa sera, sheria zetu ili kuhakikisha kwamba zinaakisi mahitaji haya yaliopo na kuhakikisha kwamba mageuzi ya kiuchumi yaliyokusudiwa na Awamu ya Nane yanafikiwa. Ni wazi kwamba tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba sheria haziwi kikwazo cha kufikia yale maendeleo ambayo tunayataka.

Mhe. Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba serikali imekusudia kuleta maendeleo ya dhati kabisa kupitia hii Awamu ya nane na mimi niseme tu kwamba kupitia mtazamo huu kuna mikataba mingi mno ambayo tutaingia. Afisi ya Mwanasheria Mkuu ina wajibu mkubwa sana wa kuhakikisha kwamba mikataba ambayo Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar itaingia iwe na tija na yenye kulinda maslahi mapana ya nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuliendea hili tunatakiwa tuwe waangalifu sana hasa katika nadharia ya maendeleo ya uchumi wa buluu kupitia sheria na mikataba yetu. Kupitia kifungu cha 56 cha Katiba ya Zanzibar ni dhahiri kwamba Mwanasheria Mkuu ndiye mshauri mkuu wa kisheria kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ni wazi kwamba tuna jukumu kubwa kama afisi ya kusimamia majukumu haya makubwa kwa maslahi mapana ya nchi yetu. Kwa hivyo, tuweke msisitizo na sisi tuna wajibu hakika wa kusimamia mikataba ambayo serikali itaingia katika maeneo ambayo nimeyataja katika ukurasa wa 10 mpaka wa 16 katika Hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pia ningependa kupitia kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu Sheria Nam. 6 ya Mwaka 2013 ambayo kwa ujumla wake imechanganua kazi za Afisi ya Mwanasheria Mkuu nazo kufikia mpaka 16. Katika kazi hizi ni kusimama kwa niaba ya serikali katika mambo ya jinai, lakini pia kuhakikisha kwamba tunakuwa na miswada yenye tija, lakini pia mikataba ambayo tunafunga tunaifunga kwa maslahi mapana ya nchi na tunaisimamia kwa maslahi mapana ya nchi yetu. Ni wazi kwamba vipengele hivyo 16 vilivyotajwa katika kifungu hiki cha 14(1) cha sheria iliyoanzisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu ni visimamio muhimu sana kwetu kuona kwamba maendeleo yanayohitajika katika Awamu ya Nane hayapati kikwazo kutokana na utekelezaji wake na zaidi kwa kuimarisha vyema Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti, tunafahamu kuna changamoto nyingi ambazo zipo lakini sisi Afisi ya Mwanasheria Mkuu tumejipanga vizuri zaidi kuhakikisha kwamba hayo yote yatakayokuja

tunayakabili kwa changamoto ambayo ilikuwepo yakiwemo mambo yafuatayo ambayo tumeona kwamba ni dhahiri ili afisi ifanye vizuri zaidi katika kazi zake ni lazima tuyafanyie kazi.

Moja ni kuimarisha kitengo cha mikataba kwa kuwajengea uwezo watendaji kwa lengo la kuongeza umahiri.

Mhe. Mwenyekiti, hili limezungumzwa kwa sauti kubwa sana na wajumbe wengi na ni wazi kwamba wanatwambia kwamba tujipange kwa huko ambako tunakwenda. Hii naweza ku-*quote* msemo mmoja wa Rais wetu Mstaafu Mzee Ali Hassan Mwinyi aliposema kwamba:

“Utakapofungua dirisha ili upate upepo tambua kwamba wataingia mpaka wadudu wengine”. Kwa hivyo, kupitia mikataba ambayo tunaingia, kupitia maendeleo ambayo tunayataka katika sekta za uchumi wa buluu na sekta nyengine wako ambao watakuja wakiwa hawana nia njema ni wazi na ni jukumu letu kuhakikisha kwamba tunakua na sheria imara na tunawajengea uwezo watu wetu ili kutambua ni mikataba gani ambayo itakuwa na tija kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imejipanga kuimarisha maadili kwa watendaji wa afisi yake pamoja na kusimamia nidhamu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2014. Lengo likiwa ni kuhakikisha kwamba tunamchukulia hatua mtu yeyote au mtumishi yeyote ambaye atakwenda kinyume na maadili na miko ya kazi.

Pia Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Mwanasheria Mkuu inajipanga zaidi kuwajengea watendaji wake kuwa wazalendo na hivyo kuweka maslahi ya nchi mbele kuliko maslahi yao binafsi. Tunafahamu mikataba hii inaingiza pesa nyingi sana na inaingiza watu ambao wana ujuzi mkubwa sana, lazima tuwajenge watu wetu kuwa wazalendo waweze kuona kwamba wanachokifanya zaidi kiwe na maslahi na nchi yetu kuliko kuweka maslahi yao binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kusema kwamba nimetoa maelezo hayo kwa lengo la kuakisi Hotuba ya Mhe. Rais ambayo kwa ujumla wake kama ambavyo mimi nimeiita ni *cyclopaedia or Speech of the Millennium* kwa sababu hakuna ambacho kimeachwa. Kwa hivyo, mimi kwa upande wangu nikiwa Mwanasheria Mkuu nimeyakisi majukumu hayo ambayo yameelezwa katika kifungu cha 14 nikiamini kwamba tuna kazi kubwa ya kufanya ili kuleta maendeleo hayo ambayo tunayatarajia.

Mhe. Mwenyekiti, kipekee kabisa na mimi nihitimishe maelezo yangu haya kabla sijakushukuru wewe niishukuru sana familia yangu, nimshukuru sana mke wangu kwa namna ambavyo daima imekuwa msaada kwangu na kwa hakika ningekuwa nimesimama hapa halafu sikutaja familia yangu yale maneno ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora nadhani naogopa kwamba na mimi ingekwenda kunikamata. Kwa hivyo, nashukuru sana mke wangu na pia familia yangu na wazee wangu nikiamini kwamba wao ndio chachu ya kuweza kufika hapa nilipofika. *(Makofi)*

Kipekee mheshimiwa nihitimishe kwa kukushukuru wewe na kukupongeza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi na kwa hakika leo hii siku yako ya mwanzo umekuwa

ukiongoza kikao hiki, nikutakie kila la kheri na mwisho niunge mkono hoja hii asilimia mia moja. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali nakushukuru sana kwa pongezi. Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi. Mheshimiwa karibu sana.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba nichukue fursa hii kuunga na Waheshimiwa Wajumbe wote waliozungumza hapa kutoa michango yao kwenye hotuba ya Mhe. Rais aliyoitoa tarehe 11 Novemba, 2020. Naomba na mimi niungane nao kwanza kwa kumpongeza Mhe. Rais na nampongeza kwa kazi zake nzuri sana kabisa, kazi za kupigiwa mfano anazoendelea kuzifanya katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025. Lakini pia kutekeleza ahadi zake alizozitoa wakati wa kampeni na ambazo anaendelea kuzitoa katika mikutano mbali mbali. Kwa kweli kazi yake na ahadi yake imejikita katika kuiletea maendeleo ya kiuchumi nchi yetu na sote tulioko hapa hatuna budi na walioko nje ya jengo hili sote tuna kila sababu ya kumuunga mkono Mhe. Rais katika kutimiza ahadi yake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais katika kipindi kifupi sana amedhihirisha kivitendo nia lakini pia utekelezaji wake katika masuala mbali mbali aliyoyaahidi na tunadhihirisha kwa kusema kwamba hivi karibuni Mhe. Rais serikali yake imesaini hati za makubaliano ya ujenzi wa bandari ya Mangapwani na bandari ya Mpigaduri, lakini pia tunashuhudia kurudi kwa nidhamu katika utendaji katika utumishi wa umma. Naungana kabisa na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria Utumishi na Utawala Bora aliposema kwamba sasa nidhamu katika utumishi wa umma imerejea na sisi sote mawaziri tunakiri kwamba hali hiyo ipo. Lakini pamoja na hayo tutazidi kuhakikisha kwamba nidhamu inabaki milele katika utendaji na utumishi wa umma.

Pia imedhihirika katika kipindi kifupi cha uongozi wa Mhe. Rais kuongezeka kwa mapato na hasa katika lango kuu la kiuchumi la bandari yetu, hilo limeelezwa na yeye Mhe. Rais kwamba mapato yameongezeka. Lakini pia tunajipongeza na tunampongeza Mhe. Rais kwamba mapato yanayotokana na utalii nayo yameanza kurudi na kuongezeka pamoja na changamoto ziliopo na Mhe. Waziri anayehusika na Sekta ya Utalii alilisema hili lakini naomba niliendeleze kwamba hata ukitizama takwimu zinatuonesha mapato katika mwezi wa Disemba yalikuwa karibu shilingi 48 milioni, yameongezeka zaidi kutoka mapato tulioyapata katika mwezi wa Novemba ya shilingi 28 milioni.

Wakati wa Corona samahani sio mapato ni idadi. Idadi ya watalii waliofika nchini kwetu mwezi wa Disemba walikuwa 48,000, lakini mwezi wa Novemba walikuwa 28,000 lakini nasema wakati wa Corona idadi ya watalii walioingia nchini kwetu ilishuka mpaka walikuwa 300. Sasa tunaona juhudi za Mhe. Rais lakini muitiko wa juhudi za serikali za kuwataka watalii kutembelea katika nchi yetu muitikio huo sasa umekuwa mkubwa na idadi ya watalii wanaofika nchini inaongezeka siku hadi siku. Lakini sio watalii tu, pia tunashuhudia wimbi kubwa sana la wawekezaji kufika nchini na kufanya mazungumzo na serikali kwa nia ya kuwekeza katika visiwa hivi. Hii inadhihirisha kwamba wawekezaji hawa wamepata hamasa kubwa sana kutokana na juhudi zinzochukuliwa na serikali ya Awamu ya Nane.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wamechangia na michango yao mimi naigawa katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza ni pongezi na wengi wametoa pongezi hizo na naungana nao kwa asilimia mia moja katika kutoa pongezi hizo. Lakini wengine wametoa pia michango ya kuonesha changamoto zilizopo katika kukabiliana na hatua mbali mbali za kufikia malengo ya kuleta maendeleo ya kiuchumi na ustawi kwa nchi hii. Eneo la tatu wametoa mapendekezo ya jinsi gani na namna ya hatua zinazofaa kuchukuliwa katika kuondokana na changamoto hizo.

Waheshimiwa wajumbe waliochangia hotuba hii au hoja hii ni 61 na niseme nilikuwepo katika Baraza hili kipindi kilichopita miaka mitano na sasa naendelea namshukuru Mwenyezi Mungu kwa mafanikio hayo haijawahi katika kumbukumbu yangu mimi kwamba hoja kupata wajumbe wengi kuchangia kama hivi. Naamini kabisa kama kungelikuwa na muda zaidi na wajumbe pengine waliobaki hao tisa au kumi nao wote wangeliweza kuchangia hoja hii.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi naomba niguse baadhi ya maeneo na nagusa baadhi ya maeneo hayo kwa sababu Waheshimiwa Mawaziri wameshagusa takriban maeneo yote, lakini niweke msisitizo wa kwamba mambo yote yaliozungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe kwanza tunayachukua na kama Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais inayohusika na Uratibu itayaratibu masuala haya ili kuhakikisha kwamba kila sekta inayazingatia na inayaweka katika mipango ya maendeleo ya kisekta ili yaweze kutekelezwa. Kwa hivyo, michango yao Waheshimiwa Wajumbe nawahakikishia kwamba itafanyiwa kazi kikamilifu.

Sasa katika maeneo ambayo nilitaka niyaguse pamoja na kwamba Waheshimiwa Mawaziri baadhi yao wameyagusa ni suala la ardhi. Niseme kwamba mengi ya haya mambo ambayo tumeyazungumza humu Mhe. Rais tayari ameshayatolea maelekezo, takriban mengi yao na yanatekelezwa na wizara mbali mbali. Kwa mfano, hili la ardhi na tumemsikia katika hotuba zake mbali mbali akisisitiza kwamba lazima tuhakikishe tuna *land bank* kwa ajili ya uwekezaji. Mhe. Waziri amesema vizuri sana suala hilo, lakini pia amekataza masuala ya kuwapa wawekezaji maeneo makubwa ambayo hawayahitaji. Sasa suala hilo nadhani sisi tulichukue kama watendaji lilizungumzwa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, Mhe. Hassan Khamis Hafidh na wewe Mhe. Mwenyekiti uliligusia suala hili. Kwa hivyo, nikuahidi kwa umoja wetu katika serikali hili tutalifanyia kazi ili kuona ardhi inayotolewa kwa wawekezaji ni ile inayohitajika kwa mujibu wa mahitaji yao ya ardhi na sio vyenginevyo.

Vile vile kuna suala jengine Waheshimiwa Wajumbe walizungumza akiwemo Mhe. Sulubu Kidongo Amour pamoja na Mhe. Juma Makungu Juma na kuwataka mawaziri tushuke chini. Hili niseme tu kwamba Mhe. Rais alilitolea maelekezo siku aliyotuapisha mawaziri wote tulitakiwa tutembelee maeneo yote na tutembelee maeneo ya wananchi kwa maana ya kuimarisha utendaji na uajibikaji na kazi hiyo inaendelea kufanyiwa kazi.

Masuala ya utalii nadhani yalizungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi kidogo Mhe. Habibu Ali Muhamed, Mhe. Issa Haji Ussi, Mhe. Bihindi Hamad Khamis, Mhe. Omar Said Shaaban, Mhe. Maryam Thani Juma, Mhe. Aza Januar Joseph na Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed. Suala la utalii lilizungumzwa vizuri sana na waziri anayehusika na utalii lakini mimi niongeze jambo moja kwamba, lile la uwekezaji katika Kisiwa cha Pemba Mhe. Rais amelitolea maelekezo na kutaka kwamba Kisiwa cha Pemba chote kiwe na upendeleo wa kwamba ni kisiwa maalum cha uwekezaji. Hivi sasa wizara inayohusika na masuala ya uwekezaji tayari wanaweka

vivutio maalum, vivutio vya *physical* na *non physical* kwa ajili ya kuvutia uwekezaji katika kisiwa cha Pemba.

Lakini katika juhudi za Mhe. Rais sote tunashuhudia kwamba hivi karibuni kuna barabara kubwa sana ya kisasa inayojengwa kuendea katika eneo huru la Micheweni na barabara ile ina karibu kilomita 12 zinawekezwa ili kuhakikisha kwamba eneo la Micheweni linafumbuka.

Suala la Uchumi wa Buluu limezungumzwa vizuri sana na Mhe. Waziri lilikuwepo suala moja la Sheria ya Uvuvi Nam.7 ya Mwaka 2010 na kuna Mheshimiwa nadhani alikuwa Mhe. Hassan Hamad Omar alizungumzia kwamba sheria ile ni kandamizi kwa wavuvi wadogo wadogo. Tunamuomba tu Mhe. Waziri atueleze maeneo ambayo yana kipingamizi kwa sababu Mhe. Rais nayo pia katoa fursa kwa sheria zote ambazo zitaonekana zina mapungufu, zina utata na zinakwamisha basi sheria hizo zianze kurekebishwa mara moja. Sasa kama kuna maeneo ambayo Mheshimiwa anahisi yanakingana na juhudi za serikali za kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo nadhani ni wakati sasa wa kuwasiliana na waziri anayehusika ili kuona sheria hiyo inafanyiwa kazi.

Lilikuwepo suala jengine la kuimarisha huduma za jamii, ambayo Mhe. Saada alitaka tuangalie kwa makini sana sera na sheria katika Sekta ya Elimu, lakini pia Mhe. Mussa Foum Mussa alizungumzia suala la kuangalia uwezo wa walimu wenyewe pia na miundombinu ya elimu. Haya nadhani yote tunayachukua kwa niaba ya Mhe. Waziri nalo tutalifanyia kazi, lakini nimwambie Mhe. Saada kwamba Mhe. Rais ametaka sera zote ziangaliwe na sheria zote ziangaliwe kulingana na mwelekeo mpya wa uchumi. Kwa hiyo, mbali ya sera na sheria zinazohusiana na Sekta ya Elimu lakini sera na sheria zote lazima sasa tuzia-*line* kutokana na mwelekeo na dira mpya ya maendeleo, dira ya 20, 50 lakini na maelekezo na mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Nane.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la miundombinu hili nitaliwacha kwa sababu naamini Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ataligusia na naamini ataligusia kwa kina, kwa hiyo naomba nimuachie yeye mwenyewe atalizungumza kwa ufanisi mkubwa.

Kuna suala la biashara na viwanda, lilizungumzwa na Mhe. Issa Haji Ussi, Mhe. Shaib Hassan Kaduara, Mhe Ali Suleiman Ameir, Mhe. Hassan Hamad Omar walizungumzia hasa suala la kukuza fursa za uwekezaji kwa viwanda vinavyotegemea malighafi lakini na viwanda tulivyonavyo kama *Azam Daily* Kiwanda cha Sukari na Kiwanda cha Basra viengweengwe na vienziwe. Hiyo ndio dhamira ya Serikali ya Awamu ya Nane na Mhe. Rais tayari ametoa maelekezo ya kuhakikisha viwanda hivi vinasaidiwa na vinaondolewa vikwazo hasa vikwazo vya masoko, lakini kwenye suala hili la Kiwanda cha Sukari tayari kuna maelekezo ya jinsi gani sukari inayotoka pale kwenye Kiwanda cha Mahonda iweze kutumika ndani na kuwafaidisha wananchi.

Kuna suala la usalama wa chakula, hili lilizungumzwa na niseme tu kwamba Serikali ya Awamu ya Nane ipo kwa kuwalinda wananchi wake na juhudi mbali mbali zinafanywa. Kwanza kutoa elimu kwa wenzetu wanaofanya biashara kuhakikisha kwamba bidhaa wanazozileta ni zile bidhaa zenye viwango, na sizo bidhaa ambazo zitakuwa na madhara kwa mtumiaji na kwa bahati mbaya wenzetu wanaoleta bidhaa ambazo zimeshapitwa na wakati na hazifai, vyombo vyetu vya

*ZFDA* pamoja na *zbs* vinafanya kazi vizuri na kuna vyakula ambavyo huangamizwa sio kwamba tunataka ifanyike hivyo lakini katika jitihada za kuhakikisha tunawalinda wananchi wetu.

Kuna suala la Mhe. Saada pia la kampuni zinazotoa mikopo bila ya leseni, mimi nimhakikishie Mhe. Saada kwamba hili wizara inayohusika Wizara ya Nchi, Fedha na Mipango italichukua na italifanyia kazi kwa kuhakikisha kwamba wale wote wanaotoa huduma za kifedha nchini basi wawe wanatoa huduma hizo kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Suala la kilimo, Mhe. Shamata Shaame Khamis, Mhe. Aza Januar Joseph, Mhe. Sulubu Kidongo Amour, Mhe. Bihindi Hamad Khamis na Mhe. Anna Athanus Paul walilizungumza kwa kina na walizungumza vizuri sana na Mhe. Waziri alilitolea ufafanuzi. Lakini niongezee kitu kidogo kwamba tuna *irrigation master plan* ambayo ilitengenezwa mwaka 2003 na tulisaidiwa na wenzetu wa *JAICA* na kama alivyosema Mhe. Waziri kuna jumla ha hekta 8561 zilionekana zinafaa kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji maji.

Lakini hivi sasa tayari serikali inaendeleza karibu hekta 1524 katika mabonde mbali mbali Unguja na Pemba, na hizi zitajumuika pamoja na zile ambazo tayari zimeshaendelezwa hekta 810 ambazo tayari zinaendelea kutumika. Kwa hivyo, nitoe shukurani za pekee kabisa kwa Serikali ya Awamu ya Saba lakini pia na ya Awamu ya Nane kwa kuendeleza juhudi hizi za kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinakuwa ni kilimo cha kisasa na hakitegemei mvua kwa sababu sasa tutakuwa na mabonde ambayo yanategemea umwagiliaji.

Mhe. Mwenyekiti, kuna masuala yalizungumzwa ya utawala bora na yalizungumzwa na waheshimiwa wengi, Mhe. Waziri aliyazungumza nitayagusa machache lakini niwashukuru sana Mhe. Saada, Mhe. Omar Said Shaaban, Mhe. Shaaban Ali Othman Mhe. Ali Abdulgulam Hussein, Mhe. Nassor Ahmed Mazurui, Mhe. Habibu Ali Muhamed, Mhe. Mhe. Hassan Khamis Hafidh wao walichangia masuala haya na kubwa walizungumzia suala la kuangalia upya nafasi ya mashirika ya umma katika maendeleo ya nchi yetu. Lakini pia Mashirika ya Umma kuimarisha uwezo wake wa kiutendaji kama Taasisi Binafsi na yalitolewa mifano mabenki hasa Benki ya Watu wa Zanzibar, lakini mashirika kuwa na mipango madhubuti ya kutafuta masoko kwa bidhaa na huduma lakini kujenga *cooperate culture* lilizungumzwa suala hilo na mashirika na taasisi huwa na mkataba wa huduma kwa umma kwa maana *customers charter* lakini pia kuwa na utambulisho kwa maana ya *values beliefs* malengo na matarajio yake.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais amejipambanua sana katika kulisimamia suala la Mashirika ya Umma na amekuwa akiguswa sana kwanini Mashirika ya Umma yawe yanaendeshwa kwa hasara akizungumza suala hasa la *Airport* na kwa kweli hakuna sababu kwamba *Airport* iwe inaendeshwa kwa hasara, lakini na mashirika mengine yawe hayatoi gawio kwa serikali.

Sasa moja ya mkakati wa Mhe. Rais na hayo ameyatolea maagizo kwamba mashirika yote ni lazima yawe yanaweza kujiendesha wenyewe, na yasitegemee ruzuku kutoka serikalini na tunaona juhudi hizo zinafanyika kivitendo kwa kubadilisha uongozi ambao utakuwa na ari na nguvu mpya katika kuleta mageuzi hayo, na kuhakikisha mashirika yetu yanatoa huduma bora, lakini pia yanatoa huduma kwa faida na kutoa gawio kwa serikali. Mfano mzuri bandari, baada ya mageuzi yaliyofanyika pale bandari tumeona sasa bandari inafanya faida kubwa sana na imekuwa na mwelekeo mzuri sana katika hilo, lakini sasa pia kumetokea mabadiliko ya uongozi

katika benki yetu Benki ya Watu wa Zanzibar, na Mhe. Rais, sote tunakumbuka mara baada ya kuapishwa ziara yake ya kwanza aliifanya pale bandarini. Kwa hivyo, tunaamini kabisa na mkazo mkubwa wa kuhakikisha mashirika haya yanafanya kazi inavyostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa na suala hili la uendeshaji wa mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *PPP* na hapa Mhe. Rais ameshapatolea maelekezo na tayari sheria inabadilishwa ile sheria ya *PPP*, ili sasa kuona miradi ya kimkakati iliyokwama kwa muda mrefu sasa inapata majibu na inatekelezwa kwa haraka kwa kuweka mazingira mazuri zaidi ya kisheria, yatakayowafanya sasa wenzetu wanaotaka kuwekeza na kushirikiana na serikali, basi wanaweza kuwasilisha mawazo yao, *proposal* zao watakaoweza kuziendeleza wataziendeleza na wale ambao watahitaji mashirikiano na serikali basi kuwe hakuna vikwazo vyovyote.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nirudie kumpongeza Mhe. Rais na kumshukuru sana kwanza kwa kutuamini baadhi yetu kumsaidia kwa karibu zaidi. Lakini naamini kwamba sote hapa tuliokuwepo ndani tuna mchango mkubwa sana wa kumsaidia Mhe. Rais kupitia majimbo yetu, na kama walivyosema wenzangu ni kwamba, sote ni washiriki katika maendeleo ya nchi yetu, tuwe mawaziri, tuwe wajumbe wa Baraza hili lakini na wananchi wote bila ya mashirikiano kazi hii inawezekana ikachukua muda mrefu lakini tukishirikiana basi maendeleo ya haraka yatapatikana na hiyo ndio dhamira ya Mhe. Rais. Naomba sana Waheshimiwa Wajumbe tuwaelimishe wananchi wetu katika majimbo yetu kuhusu dhamira ya Mhe. Rais ni dhamira ya kweli na naamini kabisa tukifanya hivyo wananchi watatuelewa na wataunga mkono juhudi hizi.

Lakini nichukue fursa hii kuwapongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais lakini pia nimpongeze Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kwa jinsi wanavyomsaidia Mhe. Rais katika kutekeleza majukumu yake, na niseme tu kwamba nawashukuru na kuwapongeza wananchi wa Donge kwa kunichagua na niwaambie kwamba hawakupoteza nafasi hiyo kunichagua kwa sababu nitatumia juhudi zangu zote na uwezo wangu wote kuleta maendeleo katika Jimbo la Donge. Lakini pia, kuleta maendeleo katika nchi nzima, kutoa mchango wangu kama waziri kwa sasa ninayehusika na masuala ya Uratibu, Sera lakini vile vile masuala ya Baraza la Wawakilishi. Naishukuru sana familia yangu yote nawashukuru kwa kuniunga mkono katika harakati zote za kisiasa, tangu nilipoingia katika shughuli hizi za kisiasa mwaka 2016 baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja Ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Waheshimiwa Wajumbe, mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo atakuwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Sasa kwa heshima kubwa naomba nimwite Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kumalizia. (*Makofi*)

**Mhe. Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kukushukuru kunipa nafasi hii lakini kwa dhati kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma Muumba Mbingu na Ardhi na vilivyomo ndani yake kutujaalia afya njema na salama nikaweza kukutana leo hii. Lakini kwa heshima kubwa napenda nichukue fursa hii kumshukuru sana Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwanza kwa kuchaguliwa kwa asilimia kubwa sana 76.2 kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Uchaguzi huu kwa wananchi umeonesha nia kubwa sana na imani kubwa sana kwa wananchi dhidi ya Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi. (*Makofi*)

Lakini la pili, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Rais Dkt. Hussein Ali Hassan kwa kuniteuwa mimi kwanza kuwa mwakilishi, lakini pia kuwa Makamu wa Pili wa Rais. Shukurani hii ni ya aina yake na kwa dhati kabisa nimuahidi sana Mhe. Rais na wananchi wote wa Zanzibar kwamba nitajitahidi kwa nguvu zote kwa kila namna kuhakikisha kwamba namsaidia sana Mhe. Rais kama malengo yalivyokusudiwa. (*Makofi*)

Lakini nimshukuru sana Mhe. Rais kwa kumteuwa Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, jambo hili naamini sana limeleta faraja kwa Wazanzibari lakini pia kuendelea kusisitiza umoja na mshikamano ndani ya nchi yetu. Nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kukuteueni Waheshimiwa Mawaziri nyote lakini bila ya kumsahau Mwanasheria Mkuu wa Serikali Dkt. Mwinyi Talib Haji lakini nikupongezeni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kuteuliwa kutoka kwenye majimbo yenu na wananchi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, hotuba hii ya Mhe. Rais ambayo imechangiwa kama ambavyo ameeleza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi na watu 61. Kwa kweli, nimekuwa nikifuatilia kwa umakini sana na kila mmoja kuona mchango wake unaelekea wapi na nini serikali tunahitajika kufanya. Hakuna mtu hata mmoja katika wote waliochangia ambaye mchango wake umeelekea kutokuridhishwa na uongozi wa Dkt. Mwinyi. Watu wote ambao wamechangia Mhe. Mwenyekiti jambo la kwanza wamempongeza Dkt. Mwinyi, hii inatafsiri Mhe. Mwenyekiti nini maana yake. Maana yake ni kwamba, kwa sababu tuliokuwepo humu ni wawakilishi wa majimbo ya Zanzibar yote, tafsiri yake ni kwamba Wazanzibari wote wanamuunga mkono Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi. (*Makofi*)

Nitumie fursa hii kuwashukuru sana Wazanzibari kwa niaba ya Mhe. Rais na kuwaahidi kwamba Serikali yetu ya Awamu ya Nane itaendelea kufanya kazi kubwa, kama kazi ambazo zimefanywa na serikali za awamu zilizopita kuhakikisha kwamba inawatumikia wananchi vilivyo. Ni dhahiri kwamba hapa ambapo Dkt. Mwinyi amechukua kijiti awamu saba zilizopita ni dhahiri kwamba zilifanya kazi nzuri, na mimi naamini Awamu hii ya Nane chini ya uongozi wa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi itafanya kazi nzuri zaidi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nikielekea kwenye michango namshukuru sana Mhe. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi amejaribu kufanya *clarification* ya maeneo mengi sana na kwa sababu na Waheshimiwa Mawaziri wote wamejaribu kutoa ufafanuzi. Mimi nitajaribu kufanya majumuisho na nitagusia maeneo lakini *in general*.

Mhe. Mwenyekiti, kama tutakuwa tumeifatilia vizuri michango ya humu Barazani, tokea tumeanza kujadili hotuba hii na hata yale maswali ambayo yalikuwa yanaelekezwa eneo kubwa ilikuwa ni Ustawi wa Jamii. Ustawi wa Jamii kwa maana maeneo mengi sana Waheshimiwa Wawakilishi wanalalamika maeneo yao hakuna maji, umeme, barabara, kilimo hakiko vizuri na shaka ya baadhi ya maeneo mengine kama suala zima la Uchumi wa Buluu ambavyo naamini baada ya maelezo ya Mhe. Waziri wananchi na wajumbe humu watakuwa wamepata uelewa mzuri sana. Mimi kwa sababu yaliyochangiwa nimeyasikia nieleze wazi ni dhahiri kwamba, wajumbe michango waliyoitoa ni kweli kabisa na ni dhahiri inahitaji kufanyiwa kazi na mimi niwahakikishie Mhe. Mwenyekiti wajumbe hao kwamba michango hiyo tutaifanyia kazi. Kwa

mfano, ukiangalia suala zima la upatikanaji wa maji Zanzibar ukienda kwa wenzetu wa Mamlaka ya Maji *ZAWA* wanasema kwamba asilimia 83 ya Zanzibar inapata maji.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ukienda kwenye uhalisia tunaipata kweli asilimia 83 ndio suala la kujiuliza, kwa sababu serikali tumekusudia kuifanyia kazi maeneo yote haya. Niwahakikishie lazima twende tukaeleze uhalisia ulivvyo kwa wananchi. Hatuna sababu ya kuwa na asilimia 83, tutafute namna wananchi waweze kupata maji kwa asilimia mia. Kama kuna shida wenzetu wa Mamlaka ya Maji, basi ni vyema mipango yao wakaileta serikalini, tukaona tunafanya nini. Lakini tukahakikisha Wazanzibari hawahangaiki na kutafuta chakula, wakahangaika na kutafuta maji, hilo jambo halitawezekana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala la upatikanaji wa maji ni jambo la lazima sio *luxury*. Naomba niwahakikishie Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, moja katika mambo ambayo ameyapa kipaumbele sana basi ni suala la upatikanaji wa huduma hizi za jamii. Kwa sababu Mhe. Waziri wa Maji na Nishati ananisikia na naamini taarifa hii anayo kabla ya mimi kusimama hapa kuisema na mawaziri wengine kwenye maeneo hayo hivyo hivyo. Nimeona pia umeme wanasema asilimia 78 na maeneo mengine wameweka zile.

Tuwache kuzungumza zile *political figure*, twende kwenye *actual*. Kama kuna shida, hakuna fedha ama kuna tatizo jengine basi jambo hilo liletwe serikalini na serikail italifanyia kazi haraka iwezekanavyo. Tusirudi katika miaka mingi ya nyuma iliyopita, mwananchi anatembea masafa marefu anatafuta maji, huo muda wa kutafuta chakula unakuwa saa ngapi.

Mhe. Mwenyekiti, hili nilitaka niliseme na nimetoa mfano mmoja tu huu wa mamlaka ya maji. Lazima turudi tukakae na wetendaji wetu, tueleze nini tatizo. Hatuna fedha, maana katika eneo ambalo unakuta miradi mengi sana imefanywa ni hapa Mjini Magharibi, miradi mingi sana ya maji imefanywa hapa lakini hata hapo Mjini Magharibi basi pia maji ni shida, yapo maeneo hayapati maji. Kwa hiyo, nilisema niliseme hili ili wenzetu, waheshimiwa mawaaziri nnamini wanafahamu lakini Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wanachi wote wanaotusikiliza wafahamu serikali yetu ya awamu ya nane tumekusudia kuelekea wapi.

Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukizingumza sana kuhusu uchumi wa buluu. Nimekuwa nikifatilia kwa karibu sana michango yote ya wajumbe. Asilimia kubwa ya michango iliyoelekezwa kwenye eneo hili iligusia zaidi kwenye uvuvi, ufugaji wa samaki, suala la mwani, maeneo hayo yaliguswa sana na mimi nafahamu kwa nini yaliguswa sana. Yaliguswa sana kwa sababu wananchi wengi wa kipato cha chini ama wanyonge wanafanya kazi hizi.

Kwa maana hiyo, Mhe. Rais alipokuwa na uono wa kuanzisha Wizara hii, amejua kabisa kwamba atasaidia kwa kiwango kikubwa suala zima hata la ajira ya watu wengi wa kipato cha chini wataweza kufanya kazi zao na kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka niseme kwa Wajumbe wa Baraza, bado suala zima la viwanda, suala zima la mafuta na gesi, matumizi mazuri ya rasilimali mbali mbali za bahari, utalii wa fukwe, bado unaingia katika suala zima la *blue economy*. Kwa hiyo, tukiweza kuyafanya vizuri haya na kama tunataka kuendelea lazima tuyafanye vizuri na mimi nakuhakikishieni kwa utaratibu na mipango ambayo Serikali ya Awamu ya Nane chini ya uongozi wa Dkt. Hussein Ali Mwinyi

inafanywa basi ni dhahiri eneo hili litatuweka kwenye *position* nzuri ya wananchi wetu lakini kuhakikisha kwamba linatusaidia katika kukuza uchumi wa nchi yetu kwa kiwango kikubwa na tukaweza kujenga uchumi mpya.

Mhe. Mwenyekiti, imezungumzwa sana bandari. Takwimu zimetolewa, hali halisi imeonesha. Kwenye bandari sitaki nizungumze zile bandari za Mpigaduri na Mangapwani zimeshatolewa maelezo vizuri. Lakini mimi hapa nitakwenda moja kwa moja kwenye ufanisi wa wafanyabiashara kupitia bandari zile. Ni dhahiri Zanzibar tumekuwa na tatizo sana kwenye eneo la bandari hasa bandari yetu ya Malindi. Kama wanakumbuka siku ambayo Mhe. Rais alikwenda pale tarehe tatu Novemba, siku moja tu baada ya kuapiswa Mhe. Rais, pale alikuta mrundikano wa makontena 1600 yamekaa pale, inasikitisha sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kufuatilia, mimi binafsi nilikwenda pale ziara mara tatu. niliwaahidi wafanyakazi wa bandari mimi nitahamia hapa. Mara ya mwisho nilipokwenda kuna kontena 410. Lakini kontena hizo ambazo alizikuta Mhe. Rais kuna kontena za toka Machi 2019 ziko pale, wakati sheria pale kontena zinakaa kwa siku 21. Zipo kontena toka 2019 Machi. Niwaombe sana wafanyabiashara wetu, tunawapenda, tunawaheshimu, tufuate sheria. Mkishindwa kufanya biashara kwa nidham ya kufata sheria tunajiuliza kuna nini. Lazima kuna kitu, hawezi kutoka hapa mpaka China, ukahangaike na ndege masaa 14 halafu urudi hapa kontena uliwache mwaka mzima Bandarini Malindi pale. Hapa kuna shida.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru Mungu mara ya mwisho nilipokwenda kuna kontena 410. Ni nikatoa *order* niletewe orodha ya majina ya wafanyabiashara ambao hawajaondoa makontena yao. Bahari nzuri siku ile nilokwenda asubuhi mpaka ilivyofika jioni zimetoka kontea 116, siku ya pili zikatoka kontena 108 na wako wafanyabiashara walikwenda mbio sana kuyatoa makontena yao pale na wengine bidhaa zilikwisha *expire*.

Mhe. Mwenyekiti, niweke wazi kabisa, Serikali ya Awamu ya Nane haitamvumilia mfanyabiashara yoyote ambae hafuati sheria. niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wafanyabiashara ni ndugu zetu, ni jamaa zetu, ni marafiki zetu na wengine inawezekana sina hakika inawezekana pengine wajumbe humu mna *share* kule. Tuhamasishaneni, tuwe wazalendo, tufuate taratibu ili tusipate shida.

Mhe. Mwenyekiti, tafsiri yangu, ukiona kontena limekaa zaidi ya miezi 6 lipo pale, aidha huyu anatafuta namna na kukwepa kodi ama kuna kitu kwa kushirikiana na watendaji kinataka kufanywa kinyume na utaratibu. Haingii akilini ukatoe kontena huko halafu uliweke pale mwaka mzima. Nawaombeni sana tuwashajihishe kwenye maeneo yetu tunaowafahamu, wafuate sheria ili wafanye kazi vizuri. Haki ambayo inastahiku kuja serikalini lazima ije serikalini na haki ambayo inawastahikia wao sisi tuko tayari waipate na kama kuna changamoto yoyote basi wakutane na mamlaka zinazohusuka, izungumzwe lakini iende kwenye utaratibu unaokubalika. Vyenginevyo, mfanyabiashara ambae atakiuka taratibu tutafuta kibali kwa mujibu wa utaribu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala zima la mapato na matumizi. Hapa Mhe. Mwenyekiti, najua muda wako umebakia mdogo sana, tutaangalia kwenye maeneo mawili. Kwanza namna ya kuongeza mapato lakini hii kabla ya kuongeza yapo mapato ambayo yamekusudiwa kukusanywa lazima

yakusanywe. Kama tumekusudia kukusanya eneo fulani kiasi kadhaa cha fedha lazima tufikie hilo lengo lakini pia tuangalie namna bora vipi tutaweza kuongeza mapato ya serikali na hili linawezekana.

Mhe. Waziri ametoa mfano wa shirika la Bandari, eneo moja tu, tumeweza. Ndani ya mwezi mmoja tumekusanya kodi ambayo ili kuwa ikikusanywa miezi 6 nyuma. Kwa hiyo, ni dhahir kwamba tunaweza.

La pili, ni namna ya kuziba mianya ya kupotea mapato. Maana hata kama unakusanya mapato, hata ukusanye kwa wingi, kama huku mfuko unavuja hayo mapato hayapo. Niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe lakini na wafanyakazi wote na wananchi kwa ujumla, kila Mzanzibari ambae ana *influence* ya kusaidia kupatikana mapato, atimize wajibu wake kwenye hilo eneo. Serikali lazima iwe na fedha na ndio tuweze kufanya hayo amambo ambayo tumeyakusudia.

Mhe. Mwenyekiti, nirudi kwenye viwanja vya ndege. Vimeelezwa vizuri lakini niseme, tuna jengo lile la *terminal 3*, nadhani si muda mrefu sana litamalizika na huduma zinategemewa zitaanza. Lengo la kwanza ni kuhakikisha tunatoa huduma bora, tuendane na usasa. Tusiwe na jengo zuri lakini huduma za kizamani. Lakini lengo la pili ni kukusanya mapato na lengo la tatu ni kuhakikisha pale tunatafuta namna na ku-*create new employment* kwa vijana wetu wapate kazi. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani na mimi nasema hapa Wajumbe wote wananisikia na haitawezekana, eneo kama bandari, eneo kama *airport* na mashika mengine yote ikawa mwisho wa mwezi tunamwambia Waziri wa Fedha na Mipango atoe fedha hazima tukalipe mshahara, haitawezekana. Haina faida. Lazima tuhakikishe kwama tunafanya kazi vizuri, tunakusanya vizuri na tunaona namna gani fedha hizo zinawafaidisha Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, nilipata fursa ya kutembelea *airport*. Nimekwenda pale zile mashine za mizigo, *checking machine* zipo 12, 9 hazifanyi kazi hiyo siku nilokwenda mimi. Lakini yupo pale sijui ndio cheo chake anaitwa nani, *DG* eee, *Director General* yupo tu pale na chumbani kwake kuna *AC* ana-*relax* tu Waheshimiwa Wajumbe *style* hii hatutafanya kazi, tutachukua hatua, wala hatutomuonea mtu muhali, hatutatizama anakotoka, hatutotizama nasaba yake, hatutatizama elimu yake, hawezi kufanya kazi akae pembeni mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie, sijui kama hii saa inakwenda sawa sawa hii, naona kama dakika zimekwenda haraka. Nimalizie suala zima la utawala bora. Nashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria amelieleza vizuri sana na mawaziri wengine wamelieleza vizuri sana, suala zima la uwajibikaji, suala zima la wizi, suala zima la uzembe, suala zima la rushwa, suala zima la ubadhirifu wa mali ya umma.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali yetu ya Awamu ya nane kwa pamoja. Tumuunge mkono Mhe. Dkt, Hussein Ali Hassan Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Kupiga vita rushwa. Kupiga vita udhalilishaji na kupiga vita uzembe. Lazima nidhamu ya serikali irudi. Imekuwa ni aibu sana na mimi nimeona hili niliseme Waheshimiwa Wajumbe, baadhi, narudia tena baadhi ya viogozi wanajaribu kutia mikono kwenye maeneo haya. Naomba nitoe tahadhari, asitafute aibu.

Wananchi wana shida nyingi, kila Mwakilishia aliyesimama hapa hakuna mmoja aliyesema mimi naunga mkono hoja jimboni kwangu hakuna changamoto. Kila aliyesimama changamoto hizo zinahitaji fedha. Sasa kama fedha hizo hazipatikani tunafanyaje, ni shida. Lazima tuhakikishe fedha hizi zinaheshimiwa, kila senti moja ya fedha ya Wazanzibari, fedha ya serikali kila mmoja aiheshimu kwa namna zote, kuanzia maofisini na hata maeneo mengine yote. Pahala ambapo kuna *single sent* ya serikali lazima iheshimiwe.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali amelizungumzia sana suala la mikataba. Limezungumzwa lakini mikataba yote ambayo haina maslahi na nchi yetu lazima iangaliwe upya.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie. Kwa sababu Mwenyekiti ananitizama sana, kuwahakikishia Wazanzibari wote. Serikali ya Awamu ya Nane itahakikisha kila mwananchi anaishi kwa upendo bila ya dhuluma ya aina yoyote ili tuweze kusogeza mbele gurudumu hili la maendeleo.

Niwashukuru sana wale wote ambao wamechangia na nnawashukuru zaidi kwa sababu wote wamemuunga mkono Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na ni dhahiri sote tunakubali kwamba Dkt. Hussein Ali Mwinyi kiboko yao. (*Makofi)*

Nimalizie kwa kukishukuru sana Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuridhia yote mpaka leo nikawa na nguvu ya kusimama hapa kama Makamu wa Pili wa Rais. Lakini namshukuru sana Mhe. Spika, Naibu Spika, Mwenyeviti wote kwa kuliendesha vyema Baraza letu bila ya kusahau na mimi kuishukuru familia yangu, wazee wangu wote, marafiki. Najua mnanisubiria nimalizie na mke wangu mpendwa pamoja na watoto wangu kwa kuendelea kunipa moyo kufanya kazi hii na wote wanasisitiza heshima kubwa ambayo serikali imenipa kila wakati niendelee kumsaidia Dkt. Ali Hassan Mwinyi. Ninawashukuruni sana wajumbe nyote nawatakieni kila la kheri. (*Kicheko)*

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na wewe kwa kunivumilia. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa ufafanuzi wa jumla. Sasa ndugu wajumbe, hoja imetolewa, naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja hiyo, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, muda uliopangwa kwa shughuli za asubuhi umeisha. Kabla ya kuelekea kuakhirisha, naomba nisome matangazo mawili, yote yanatoka kwa Mnadhim, ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Baraza la Wawakilishi wa CCM, wabakie mara baada ya kuakhirishwa kwa kikao hiki.

Tangazo la pili, Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wenye majimbo wanatakiwa kupeleka majina ya kamati zao za Maendeleo ya Majimbo pamoja na *account* za Mfuko wa maendeleo ya majimbo kwa ajili ya utaratibu wa kuingiziwa fedha za mfuko wa jimbo katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kabla ya tarehe 20/2/2021.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa nimwite Mhe. Wakazi wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa ajili ya kutoa hoja ya kuakhirisha Kikao chetu cha Baraza hadi kesho saa 3:00 asubuhi. Mhe. Waziri karibu.

**KUAKHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE**

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja ya kutengua Kanuni ya 23, ili uweze kuliakhirisha Baraza lako kwa madhumuni ya kumpa fursa zaidi Mhe. Waziri anaehusika na Masuala ya Fedha na Uchumi, kujitayarisha kuwasilisha Muelekeo wa Mpango wa Taifa kwa mwaka 2021-2022 na Waraka wa Mpango wa Bajeti.

Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa, sasa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, kwa tafsiri hiyo, sasa naomba kuakhirisha shughuli za Baraza hadi kesho saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 7:04 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 16/02/2021 saa 3:00 asubuhi)*